BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,012,798,111/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Saa zahesabika hukumu ya kina Mdee korti kuu**

UKURASA 2



**JORGINHO HATAKI KUONDOKA CHELSEA**

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Julai 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580999 *

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


ZIBA

# Shule ya kata iliyopindua meza matokeo kidato sita

• **2019** ilikuwa hoi, Mkuu wa Shule afunguka siri ya mapinduzi... *Ukurasa 4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### VIGOGO CCM WAJITOKEZA KUWANIA NAFASI UONGOZI

VIGOGO wa Chama Cha Mapundizi (CCM), wamejitokeza kugombea nafasi za uenyekiti wa mkoa na wilaya, huku wengine wakitetea nafasi zao na...

UKURASA WA 7

### WACHUMI WAFUNGUKA KUPANDA BEI YA MAFUTA

SIKU moja baada ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (UWURA), kutangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta...

UKURASA WA 7

### ANAYESHTAKIWA KUKUTWA NA NYETI ZA KIKE 5 ADAIWA KUZIPELEKA RUFIJI

MKAZI wa Maswa, Salum Nkonja (23), anayetuhumiwa kukutwa na sehemu za siri tano za mwanamke na chuchu tano...

## Kinana ashtuka lugha Kiswahili kutoinufaisha Tanzania

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam kabla ya kuanza safari kwenda Dakar, Senegal kuhudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika zinazonufaika na Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Mamilioni ya Shirika la Jiokoe Umaskini yaibwa

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YAANZA HESABU ZA CAF** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mamilioni Shirika Jiokoe na Umaskini yaibwa

**Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MTU asiyejulikana amevunja na kuiba fedha taslimu na vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 7,760,000 mali ya Shirika la Jiokoe na Umaskini yaani Stars of Poverty Rescue Foundation (SPRF) zilizoko katika Manispaa ya Singida mkoani hapa.

Mkurugenzi Mtendaji wa SPRF, Dk. Suleiman Muttani, alisema jana kuwa tukio hilo limetokea Juni 26, mwaka huu, kati ya saa 11:30 na 12:00 jioni katika ofisi hizo zilizoko kati ya ofisi za mkoa za kampuni ya simu ya Tigo na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kata ya Ipembe.

Alisema taarifa za tukio hilo ambalo mtuhumiwa alinaswa na camera za CCTV wakati akiiba, limeripotiwa katika Kituo Kikuu cha Polisi Singida na kusajiliwa kwa namba SGD/IR/3240/2022.

Dk. Muttani alivitaja vitu vilivyoibwa kuwa ni kompyuta mpakato (laptop) aina ya HP, runinga ya inchi 36, projecta aina ya Epson, 'hard disc mbili zenye ukubwa wa GB 500 na GB 1000 na fedha taslimu Sh. milioni mbili ambazo zilikuwa zimewekwa ofisini kwa ajili ya kulipia kodi ya pango la ofisi.

Kwa mujibu wa Dk. Muttani, mwizi huyo ambaye ameonekana kwenye kamera akiwa amevaa kofia, shati jekundu, koti jeusi na suruali nyeusi kabla ya kuiba, alivunja milango mitano ambayo ni ya kuingilia getini, kliniki na ofisi za utawala za SPRF.

Pia alisema mwizi huyo alinyofoa baadhi ya camera za CCTV lakini zingine zilizobaki ambazo hakuziona, zilimnasa wakati akitekeleza wizi huo.

"Mwizi huyo baada ya kufanikisha uhalifu huo alichukua funguo za ofisi na kuzipanga juu ya viti ambavyo wanaketi watu wanapokuja kufuata huduma za matibabu," alisema.

SPRF ni Shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na kupunguza umaskini na kuleta maendeleo, kutoa huduma za afya na kufanya utetezi wa haki kuhusu usawa wa kijinsia na haki za wanawake, watoto na makundi mengine athirika.




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kulia), akimsikiliza Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mishipa ya Hepatobiliary kutoka Child Life Ufalme wa Bahrain, barani Asia, Prof. Martin Corbally, aliyeongoza timu ya wataalamu kuwatenganisha pacha walioungana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es Salaam alipowatembelea watoto hao jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Saa zahesabika hukumu kina Mdee

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Masijala Kuu imeshindwa kutoa uamuzi wa maombi ya Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, na wenzake 18 ya kibali cha kuwasilisha mapitio ya kimahakama wakipinga kuvuliwa uanachama wa CHADEMA, kwa kuwa uamuzi huo haujakamilika.

Katika taarifa yake jana, Msajili wa Mahakama Kuu, Elimo Masawe, alisema uamuzi haujakamilika na hivyo shauri hilo limeahirishwa hadi Ijumaa, yaani kesho saa sita mchana.

Uamuzi huo ulitarajiwa kutolewa na Jaji Mustapha Ismail ambapo waleta maombi (Mdee na wenzake) waliwasilisha hoja tano za kisheria kuishawishi mahakama itoe kibali hicho kwa kuwa maombi hayo waliyafungua ndani ya muda.

Wakati wakiwasilisha hoja zao, Wakili wa Mdee na wenzake, Ipilinga Panya, alidai wamewasilisha ombi hilo wakiwa na hoja tano ikiwamo ya kwamba wamefungua maombi hayo ndani ya muda wa kisheria.

Alidai hoja nyingine ni kuonyesha kuna jambo linalobishaniwa, kuonyesha maslahi ya waleta maombi, CHADEMA ni chombo cha umma na kama walitafuta haki zao ndani ya chama hicho.

Wakili Panya alidai maombi hayo yamefunguliwa kwa wakati kwa kuwa yalitakiwa yaombwe ndani ya miezi sita tangu kutolewa kwa uamuzi unaolalamikiwa na hivyo Mdee na wenzake wamefungua maombi yao ndani ya muda.

Alidai waleta maombi wote ni wabunge wa viti maalum walioteuliwa na Bodi ya Chama hicho mwaka 2020-2025, hivyo uamuzi wa kuwafukuza uanachama bila kufuata utaratibu wa kuwasikiliza, unagusa maslahi yao binafsi.

Wakili Panya alidai Mdee na wenzake wana maslahi mapana katika jambo hilo, wameathirika na uamuzi wa bodi hiyo kupitia uamuzi wa Baraza Kuu la Chama hicho wa Mei 11, 2022 uliowafukuza uanachama.

Wakili Peter Kibatala katika kujibu hoja hizo, alidai hawabishi hoja kwamba Mdee na wenzake wana maslahi mapana ila kigezo cha mgogoro hakiangaliwi juu, bali lazima kuwapo ushahidi mahakamani chini ya kiapo ili mahakama ichunguze na hawajauwasilisha.

Alidai hawabishi kwamba waleta maombi kwenda mahakamani, lakini njia waliyotumia ilikuwa si sahihi, kwa kuwa walichelewesha haki zao kwa kuiomba mahakama kwa njia ya mapitio.

Wakili Kibatala alidai watu 28 hawawezi kubadili uamuzi wa wajumbe 437, waleta maombi walikuwa wanaijua Katiba ya Chadema na kwamba wajumbe wa Kamati Kuu wanaingia katika Baraza Kuu, hivyo haikuwahi kuleta shida, haiwezi kuwa hoja ya msingi.

Kibatala alidai kwamba CHADEMA siyo chama cha umma na hakifanyi kazi za umma kama ilivyoelezwa na waleta maombi.

Mdee na wenzake walifungua kesi hiyo dhidi ya Baraza la Wadhamini la CHADEMA, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

# RC Mbeya atafuta dawa kuepusha ajali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameagiza Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) mkoani humo kujenga kituo cha malori kukaguliwa katika eneo la Inyala katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ili kuepusha ajali za mara kwa mara.

Homera alitoa agizo hilo jana ikiwa ni siku moja baada ya lori la mizigo lililokuwa limesheheni magunia ya mahindi likitokea mkoani Songwe kwenda jijini Dar es Salaam kushindwa breki katika eneo hilo na kuligonga basi dogo la abiria.

Katika ajali hiyo watu watano walifariki dunia papo hapo na wengine ambao idadi yao haikutajwa kujeruhiwa huku likiharibu vibanda vya wajasiriamali, miundombinu ya umeme na kuvamia nyumba za watu zilizoko pembezoni mwa barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Akizungumza na wandishi wa habari ofisini kwake jana, Homera alisema ajali zinatokea mara kwa mara katika eneo hilo kutokana na mteremko kuwa mkali na magari mengi hasa ya mizigo kushindwa breki.

Alisema ili kudhibiti ajali hizo wameamua kuweka utaratibu wa magari makubwa na madogo kupita kwa awamu kama walivyofanya katika maeneo mengine ikiwamo mteremko wa Mlima Lwambi, Igawilo na Mlima Nyoka.

Alisema malori yatakuwa yanasimamishwa katika eneo hilo kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi kabla ya kuanza kuteremka na yanapoanza kushuka magari madogo yatakuwa yanasubiri ili hata ikitokea tatizo madhara yanakuwa madogo.

"Nimeshamuagiza Meneja wa TANROADS na ameshawatuma vijana wake wapo eneo la tukio wanaandaa eneo kwa ajili ya kujenga kituo hicho, hatuwezi kukubali ajali ziendelee kuua watu maana juzi tu hapa Meneja wa Benki ya NMB alifariki katika eneo hilo na jana (juzi) tena watu watano wanafariki na wengine wengi kujeruhiwa," alisema Homera.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema majeruhi wa ajali hiyo walipelekwa katika hospitali tofauti za mkoa huo ikiwamo Hospitali ya Inyala, Igawilo na Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Alisema ili kudhibiti ajali hizo wanaendelea kuwasiliana na wadau wengine ili kuangalia namna ya kudhibiti ajali huku akieleza kuwa eneo hilo barabara yake ni nyembamba kiasi kwamba magari yanashindwa kupishana vizuri.

"Tunawaomba wenzetu TANROADS watusaidie kupanua barabara hii ili magari yawe yanapishana vizuri na hata kukitokea dharura kuwe na namna ya kuokoa maisha ya Watanzania," alisema Matei.

Hata hivyo, jana Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, aliwatembelea majeruhi wa ajali hiyo waliolazwa katika hospitali hiyo na alithibitisha kuwa wanaendelea vizuri.

Alisema katika hospitali hiyo walipelekwa wajeruhi saba ambao kati yao watano ni wanawake na wengine wawili ni wanaume na kwamba wote hali zao zinaendelea kuimarika.

HABARI KITAIFA

# Kisena kizimbani kwa mara ya tatu

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa SGR na Kampuni ya Huduma za Usafirishaji wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (Udart), Robert Kisena (47), amepandishwa tena kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa mara ya tatu akikabiliwa na mashtaka 25, likiwamo la kusababisha hasara ya Sh. bilioni 4.4.

Katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 20/2022, Kisena anatuhumiwa kuisababishia Udart hasara ya Sh. milioni 750 na kesi namba 21/2022 anatuhumiwa kutakatisha fedha Sh. bilioni 4.5.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Timotheo Mmari akisaidiana na Yusuph Aboud, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, alidai kwamba katika kesi hiyo, mbali na Kisena, washtakiwa wengine ni Mkurugenzi wa Simon Group Ltd, Charles Newe (48) na Mfanyabiashara Kulwa Kisena (34).

Alidai washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 25. Kati yake, 22 ni ya wizi wakiwa wakurugenzi, kuongoza genge la uhalifu, kuisababishia hasara Udart na kutakatisha fedha.

Alidai kuwa katika shtaka la kwanza, watuhumiwa wote kwa pamoja kati ya Septemba 15/2017 na Januari 31, 2019, wakiwa sehemu tofauti ndani ya Jiji na Mkoa wa Dar es Salaam, kwa makusudi waliongoza genge la uhalifu na kujipatia Sh. bilioni 4.4 kutoka akaunti ya Udart ya benki ya NMB tawi la Benki House.

Katika shtaka la pili, Mmari alidai kwamba Septemba 29, 2017 washtakiwa wakiwa katika benki hiyo kama wakurugenzi na Ofisa wa Udart, kwa manufaa yao binafsi walihamisha Sh. milioni 287, mali ya Udart.

Mmari alidai katika shtaka la kuisababishia hasara Udart, inadaiwa kati ya Septemba 30/2017 na Januari 31/2019, ndani ya Jiji na Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa wakiwa wakurugenzi na Ofisa wa Udart, kwa makusudi waliisababishia hasara Udart Sh. bilioni 4.4.

Inadaiwa kwamba tarehe hizo hizo washtakiwa wakiwa wakurugenzi na ofisa wa Udart walijipatia Sh. bilioni 4.4 huku wakijua fedha hizo zimetokana na mazalia ya kosa la wizi.Baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka yao, Hakimu Shaidi aliwaeleza kwamba kesi yao ni ya uhujumu uchumi, hawatakiwi kujibu chochote, ambapo Wakili Mmari alidai upelelezi umekamilika na kilichobakia ni kuwasilisha taarifa Mahakama ya Mafisadi ili kesi isikilizwe.

Wakati Kisena na wenzake wanasomewa mashtaka yao, walikuwa wakifuatilia kwa makini kwenye hati ya mashtaka na muda mwingine kwa sauti za chini walikuwa wakielekezana.

Ilipofika muda wa kupanga tarehe ya kesi kutajwa, Kisena alidai kwamba anataka kuieleza mahakama kama itaona inafaa, kesi ipangiwe kutajwa Julai 18/2022 kwa sababu tarehe hiyo wana kesi zingine mbili.

Hakimu Shaidi akamhoji Kisena kwa nini anataka iwe hivyo, Kisena akadai kwamba huwa kuna shida ya usafiri wa kutoka gerezani kwenda mahakamani.

Hakimu akamuuliza Ofisa Magereza aliyekuwa kwenye chumba cha mahakama kama ni kweli kuna shida hiyo, akadai magari yao yapo. "Kesi kuja hapa ni kwa mujibu wa sheria, kwa hiyo msiwaonee huruma hawa, Magereza wapo kwa ajili yenu, haya ninaahirisha kesi hadi Julai 18, 2022," alisema Hakimu Shaidi.



Nyumba zikiwa katika mazingira ya hatari baada ya udongo kuondolewa kwa ajili ya upanuzi wa barabara unaoendelea, eneo la Kimara Korogwe Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kinana ashtuka Kiswahili kutoinufaisha Tanzania

**Na Jenifer Gilla**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, amesema licha ya Tanzania kuwa mwasisi wa Kiswahili, hainufaiki na lugha hiyo kiuchumi badala yake nchi zingine kama Kenya ndizo zinazonufaika.

Kinana aliyasema hayo Dar es Salaam katika mdahalo wa maadhimisho ya Siku ya Mchango wa Lugha ya Kiswahili katika Ukombozi wa Bara la Afrika ulioandaliwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kilele cha maadhimisho hayo kinafikia leo.

"Kwa bahati mbaya, sisi si wafaidikaji wakubwa wa Kiswahili duniani. Dunia nzima wafaidikaji wakubwa ni wengine, siyo Tanzania. Mapato yanayotokana na matumizi ya lugha ya Kiswahili duniani ni dola bilioni 1.3. sasa jiulize sisi Watanzania tunapata kiasi gani? Alihoji.

Alisema mapato hayo yanatokana na wanafunzi, wakufunzi, wakalimani, redio na runinga za Idhaa ya Kiswahili huku taasisi 72 duniani zikifundisha lugha hiyo, Marekani pekee ikiwa na taasisi 122 na China tatu zinazofundisha lugha hiyo huku wanaofanya shughuli hizo wengi wakitoka nchi zingine ikiwamo Kenya.

Kinana ambaye alishiriki katika harakati za ukombozi wa Afrika, alisema wanazungumzia mchango wa lugha hiyo Afrika, wanajiangalia wao kwanza kwa sababu imechangia kuleta umoja wa kitaifa uliopo kwa kuwa ndiyo lugha inayotumika kwa mawasiliano tangu enzi za kutafuta Uhuru na kuharakisha kupatikana kwa ukombozi.

"Na moja ya chombo kilichosaidia ukombozi wa Tanzania, kupatikana kwa Uhuru mapema ni lugha ya Kiswahili pamoja na shughuli nzima ya ukombozi. Kwa nini? Kwa sababu wote tulikuwa tunazungumza Kiswahili. Viongozi na wananchi walikuwa wakiwasiliana kwa Kiswahili, vyombo vya habari vilikuwa vinazungumza Kiswahili. "Wote ni mashahidi kwamba Baba wa Taifa (Julius Nyerere) na viongozi wenzake wa Chama cha TANU wakati ule, walizunguka nchi nzima mikoa kwa mikoa, wilaya kwa wilaya, vijiji kwa vijiji kuzungumza na Watanzania juu ya harakati za ukombozi wa nchi yetu. Na jambo hili lilimsaidia sana. Watanzania waliwaelewa viongozi haraka na tuliweza kupata uhuru wetu mapema sana," alisema Kinana.

Lugha hiyo, alisema, pia imesaidia katika harakati za ukombozi kwa baadhi ya nchi za Afrika zikiwamo Msumbiji, Rwanda na Uganda ambayo hivi karibuni imetangaza kutumia lugha hiyo rasmi.

"Raia wengi wanaoishi kaskazini mwa Msumbiji wanazungumza Kiswahili na huko ndiko kulikoanzia mapambano ya ukombozi, katika Jimbo la Cape Delgado, ambalo linapakana na Tanzania. Kwa hiyo ilikuwa rahisi kutumia lugha ya Kiswahili kuanzisha ukombozi," alisema.

Kinana alisema hata baada ya ukombozi, Kiswahili kilisaidia kujenga ujirani mwema baina ya Tanzania na nchi zinazopakana nayo kama vile Kenya, Uganda na Rwanda ambazo wananchi wake wana ukaribu zaidi tofauti na nchi ambazo hazizungumzi lugha hiyo.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, akisoma risala ya Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alisema nchi za Afrika zinapaswa kutumia lugha hiyo kujiletea maendeleo ya kiuchumi kama ilivyoitumia katika harakati za kujikomboa kifikra.

"Kama tuliweza kutumia lugha hii kushikamana na kujijenga kifikra na hatimaye kuwaondoa wakoloni, basi tutumie nafasi hii kwa kasi na nguvu ile ile kukitumia Kiswahili kujikomboa kiuchumi," alisema.

Pia alisema kuwa kazi kubwa waliyo nayo Wizara na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) ni kuhakikisha kuwa wanaiuza lugha ya Kiswahili nje ya mipaka ya nchi ili kuchangia katika pato la taifa na kukuza uchumi wa nchi.

Vilevile aliwasihi vijana kuachana na kasumba ya kutumia lugha ya kigeni kwa tafsiri ya kuonekana kuwa ni wasomi au watu wenye maendeleo na kutoa wito wa watafiti kuandika na kutafsiri historia ya nchi hiyo kwa Kiswahili ili jamii ijue wao ni nani na wametokea wapi kwa kuwa historia ya nchi hiyo imefichwa kwenye lugha za kigeni.

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PENDO SISTY CHUWA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – SALASALA | LEGENDS AUCTION MART | 21-07-2022 |
| 2 | WINJONES FAUSTINE MNG'ANYA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KILUVYA | LEGENDS AUCTION MART | 21-07-2022 |
| 3 | MODESTUS IBRAHIMU MELEO | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – MBAGALA | LEGENDS AUCTION MART | 21-07-2022 |
| 4 | ESTHER MOSSES FIKIRINI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KINYEREZI | JOFORTE AUCTION MART | 21-07-2022 |
| 5 | DOREEN DANIEL MAJULA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - GOBA | JODAC PROFESSIONALS CO LTD | 21-07-2022 |
| 6 | SWEDY KHAMIS SWEDY | PAGALE | HATI YA MAKAZI - KIGOGO FRESH | LEGENDS AUCTION MART | 21-07-2022 |
| 7 | MARY DAVID KINONG'O | GARI | TATA LPT TRUCK - T 250 DKR | JODAC PROFESSIONALS CO LTD | 21-07-2022 |
| 8 | SELESTINE CLEMENCE KATO & MARYSTELLA SELESTINE KATO | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – CHARAMBE | JODAC PROFESSIONALS CO LTD | 21-07-2022 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

216934902

MAKALA MAALUM



ZIBA

# Shule ya kata iliyopindua meza matokeo kidato 6

Na Sanula Athanas

MWISHONI mwa mwaka 2019, nilizuru kwenye Shule ya Sekondari Ziba. Safari yake kwa gari inachukua takriban saa 15 kuifikia, umbali wa Km 876.7 kutoka jijini Dar es Salaam.

Mahali ilipo shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 2000, ni umbali wa Km 57 magharibi mwa Mji wa Igunga mkoani Tabora.

Nilipowasili shuleni huko, nilishuhudia ugumu uliokuwa unawakabili walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji, shida kuu ikiwa ni uhaba mkubwa wa walimu.

Kipindi hicho shule hiyo ilikuwa inajiandaa kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano, lakini wadogo zao, kwa maana ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne walikuwa na kitendawili kigumu kuyamudu masomo, hasa ya sayansi, baadhi yakiwa hayana walimu kwa miaka minne mfululizo.

Mathalani, somo la Fizikia, kitendawili kigumu kilionekano kuwa dhahiri, nilishuhudia shule hiyo haikuwa na mwalimu wa somo hilo kwa miaka minne mfululizo kutoka mwaka 2015 hadi 2019.

"Hapa hatuna mwalimu wa Fikizia aliyeajiriwa na serikali kwa miaka minne sasa. Shule ilianzishwa mwaka 2000. Awali, alikuwapo Mwalimu Kabahoze aliyekuwa ameajiriwa na serikali kwa ajili ya somo hilo, lakini mwaka 2015 alipandishwa kuwa MEK (Mratibu Elimu Kata) na hakuajiriwa mwalimu mwingine kuziba pengo hilo," Makamu Mkuu wa Shule hiyo (mwaka 2019), Frank Milazi, alibainisha.

Kilio cha Mwalimu Milazi kiliendа mbali zaidi, akilalamika kwamba uhaba huo pia ulikuwa unaangukia masomo ya Kemia na Baiolojia, ambayo ndiyo wabia wakuu wa Fizikia katika sayansi, kila somo kipindi hicho lilikuwa na mwalimu mmoja.

Kisera, inaainishwa kwamba tija ya mwalimu na mzigo unaobebeka kwake ni anapokuwa na wastani wa wanafunzi 45 kwa darasa. Shule ya Sekondari Ziba kipindi hicho ilikuwa na walimu 16, waliotakiwa kufundisha wanafunzi zaidi ya 900 wa kidato cha kwanza hadi cha nne, huku shule hiyo ikiwa mbioni kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano.

Kimiundombinu, Nipashe ilibaini kwenye shule hiyo kulikuwa na nyumba tatu tu kwa ajili ya walimu, hivyo walimu wengi wa shule hiyo walilazimika kutafuta makazi mitaani.

Katika kutekeleza wajibu wake, Desemba 31, 2019, Nipashe ilichapisha ripoti maalum yenye kichwa cha habari 'UHABA WA WALIMU JANGA ELIMU NCHINI', ikiwa na ushuhuda wa kilichokuwa kinajiri katika Shule ya Sekondari Ziba.

Siku chache baada ya kuchapishwa kwa ripoti hiyo ambayo ilitambuliwa kuwa miongoni mwa kazi bora zaidi katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa Mwaka 2019, serikali ilichukua hatua kadhaa zikijumuisha kupeleka walimu kwenye shule hiyo, baadhi wakihamishwa kutoka katika shule zilizokuwa na idadi kubwa ya walimu.

Vilevile, Mbunge wa Manonga inakopatikana shule hiyo, Seif Gulamali, alitekeleza wajibu wake wa kutetea maslahi ya wananchi, akizuru mara kwa mara kwenye shule hiyo akiwa na mawaziri husika (Elimu na TAMISEMI).

Jitihada hizo zikazaa matunda - kukajengwa mabweni, nyumba za walimu, bwalo la chakula, madarasa mapya, vyoo na viwanja vya michezo, ukiwamo wa mpira wa miguu ambao mbunge huyo amehakikisha unakuwa na majukwaa kwa ajili ya watazamaji.

**WAPINDUA MEZA**

Uwekezaji unalipa! Jitihada za wadau hao wa elimu hatimaye zimezaa matunda, Shule ya Sekondari Ziba ikitangazwa juzi kuwa miongoni mwa shule 10 bora kitaifa katika matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita mwaka huu.

Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) lilibainisha orodha hiyo yenye shule saba za serikali, ina shule mbili za kata. Mbali na Ziba, shule nyingine ya kata iliyopindua meza na kuziangusha shule kongwe na zinazomilikiwa na taasisi binafsi, ni Shule ya Sekondari Mkindi iliyoko wilayani Kilindi mkoani Tanga.

Orodha kamili ya shule 10 bora kitaifa ni; Kemebos (Kagera), Kisimiri (Arusha), Tabora Boys (Tabora), Taboora Girls (Tabora), Ahmes (Pwani), Dareda (Manyara), Nyaishozi (Kagera), Mzumbe (Morogoro), Mkindi (Tanga) na Ziba (Tabora).

**SIRI YA MAPINDUZI**

Mkuu wa Shule hiyo, Ally Nohoye, katika mazungumzo na Nipashe jana, alisema siri ya mafanikio hayo ni kujituma kama timu, mshikamano, wanafunzi kukujifunza kwa bidii na kujenga kuaminiana.

Alibainisha kuwa kabla ya kufanya mitihani, walimu na wanafunzi walikuwa kitu kimoja na kulikuwa na ushirikishaji wa wazi katika kufundisha, kuendesha mijadala na kurekebisha makosa katika masomo yote.

Alisema kwamba katika mkakati wao huo, walimu walijipanga kuhakikisha wanakuwa karibu na wanafunzi wote ili kujua matatizo yao katika uelewa wa masomo kwa kila mmoja.

"Tuliondoa ombwe kati ya walimu na wanafunzi, sisi kama walimu tulishikamana kuhakikisha kila mwanafunzi tunajua matatizo ya uelewa kwa kila somo, tukibaini tunakaa kulitatua, tukimshirikisha na mtoto mwenyewe," alisema.

Mwalimu Nohoye alisema kuwa kwenye mkakati huo, wote kwa pamoja walikuwa na kauli moja ya kuipandisha shule yao kutoka nafasi ya 47 mwaka jana hadi kuingia 10 bora.

"Kila mmoja alitambua nini tunahitaji, walimu na wanafunzi wote walitambua jambo gani linawakabili kwa wakati huo, tunamshukuru Mungu ametusikia na kutufikisha hapa tulipo sasa.

"Tunawashukuru wanafunzi kwa kutuelewa nini wanatakiwa kufanya, walituelewa na ndiyo maana katika masomo na mijadala hakukuwa na matatizo, walisaidiana wenyewe kabla ya kufika kwetu," alipongeza.

Alisema darasa hilo limeacha kumbukumbu nyingi kutokana na usikivu wao, akikumbusha kuwa ilifikia wakati kila mwanafunzi alimwona mwenzake kama ndugu na hakutaka kuona anaanguka katika masomo.

"Tuliwajenga wajione kama familia moja, mmoja akianguka mwenzake aumie, hata katika makundi yao ya mijadala au masahihisho, mmoja akikosa tuliliadhibu kundi lote ili watambue maana ya umoja," alisisitiza.

Mwalimu Nohoye alisema matokeo hayo kwa walimu wanajiona kama wameanza kutembea, hivyo wanahitaji kukimbia ili kushika nafasi za kwanza kitaifa.

Akizungumzia vikwazo vinavyoikabili shule yake, Mwalimu Nohoye alisema ukosefu wa ofisi za utawala, jengo la maabara na uhaba wa nyumba za walimu.

Aliiomba serikali kuhakikisha inaboresha zaidi mazingira ya shule hiyo kwa kuongeza majengo hayo na hasa nyumba kwa ajili ya walimu ili wawe karibu zaidi na wanafunzi na kutatua matatizo yao kwa haraka.

Kwa mujibu wa NECTA, Shule ya Sekondari Ziba ilikuwa na watahiniwa 74 katika mtihani huo wa kidato cha sita. Kati yao, 71 wamepata daraja la kwanza huku wanne wakifaulu kwa daraja la pili. Mchanganuo zaidi unaonyesha wasichana walikuwa 27 (wote wamefaulu kwa daraja la kwanza) na wavulana walikuwa 47 (44 wamefaulu kwa daraja la kwanza na watatu wamepata daraja la pili).

# Rais Samia atoa pole waliovamiwa na tembo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan (pichani) ametoa pole kwa wananchi kutokana na athari walizozipata baada ya tembo kuvamia katika vijiji vyao na kusababisha maafa kikiwamo kifo.

Salamu hizo zilitolewa jana na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa niaba ya Rais Samia, wakati akizungumza na wananchi katika kijiji cha Nditi.

Waziri Mkuu alifanya ziara wilayani Nachingwea kwa ajili ya kukagua athari zilizosababishwa na uvamizi wa tembo katika mashamba ya wananchi kwenye kijiji cha Namapwiya na kuwapa pole wananchi hao.

Alisema Rais Samia anawapa pole kutokana na athari hizo na kwamba serikali itahakikisha hakuna mwananchi atakayekosa chakula.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea kupitia kamati ya maafa ya wilaya ahakikishe wanaandaa utaratibu wa kupatikana chakula kwa wananchi wote ambao mashamba yao yameathiriwa na wanyamapori.

Alisema tatizo hilo limechangiwa na wafugaji kuvamia maeneo ya hifadhi kwa kuingiza mifugo ikiwamo mbuzi, ng'ombe na kondoo katika hifadhi na kusababisha wanyamapori kukimbia kwenda kwenye makazi ya wananchi.

Kutokana na hali hiyo Waziri Mkuu alimwagiza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki kukutana na wafugaji na kuwataka kutopeleka ng'ombe na mbuzi kwenye maeneo ya hifadhi.

Pia Mheshimiwa Majaliwa alitoa wito kwa wananchi kutoingia na kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo ya hifadhi ili kuepuka mazao yao kuharibiwa na wanyamapori.

Alisema katika kuhakikisha wanyamapori wanadhibitiwa, Rais Samia ameridhia zaidi ya Sh. bilioni 1.2 zitumike kwa ajili ya ujenzi wa vitu 19 vya askari wa wanyamapori karibu na maeneo ya hifadhi.

Alisema kati ya vituo hivyo vitatu vitajengwa katika wilaya tatu za mkoa wa Lindi ambazo ni Nachingwea (Nditi), Liwale (Liwale) na Milola (Ruangwa).

Vilevile, alisema Rais Samia ameridhia kibali cha ajira 6,000 askari wa wanyamapori ambao watasambazwa katika maeneo yote yanayopakana na hifadhi.

Ajira hizo zinalenga kuendelea kuimarisha ulinzi na kudhibiti wanyamapori kuingia kwenye maeneo ya makazi ya wananchi. "Tunataka wananchi waendelee kuishi kwa amani."

Alisema serikali imetoa namba ya bure ya mawasiliano ambayo ni 0800110067 ili kuwawezesha wananchi kutoa



taarifa mara wanyamapori wanapovamia kwenye makazi yao.

Akiwa katika kata ya Nditi kijiji cha Namanja kabla ya kuzungumza na wananchi, Waziri Mkuu alikwenda kuifariji familia ya marehemu Riziki Issa, ambaye aliuawa na tembo.

Akizungumza kwa niaba ya familia hiyo Mussa Nambole alisema wamefarijika viongozi mbalimbali wa serikali walivyoshirikiana nao kipindi cha msiba huo.

Naye Mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chingwile, aliishukuru serikali kwa kuweka mikakati mbalimbali inayolenga kuzuia uvamizi wa wanyamapori kwenye makazi ya wananchi.

# Vigogo CCM wajitokeza kugombea uongozi

**Na Waandishi Wetu**

VIGOGO wa Chama Cha Mapundizi (CCM), wamejitokeza kugombea nafasi za uenyekiti wa mkoa na wilaya, huku wengine wakitetea nafasi zao na waliokuwa kwenye nafasi hizo wakirudi. Makada hao 16 ni wa mkoa wa Shinyanga na Tarime, waliogombea nafasi tofauti ndani ya chama hicho.

Aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Hamisi Mgeja, jana alichukua fomu ya kuwania nafasi hiyo.

Mgeja alikuwa Mwenyekiti wa CCM, mkoani Shinyanga, mwaka 2007 hadi 2015 kabla ya kuhamia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na baadaye kurudi tena kwenye chama chake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye ofisi za CCM mkoani Shinyanga baada ya kuchukua fomu ya kugombea nafasi hiyo, alisema amejitathmini na kuona anafaa tena kuwa kiongozi, na kwamba ni haki yake ya kikatiba kugombea.

"Nimekuja kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya wanachama mkoa wa Shinyanga baada ya kujitahmini na kuona naweza tena kuwa kiongozi na nimetumia haki yangu ya kikatiba kama mwanachama wa CCM," alisema Mgeja.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa, alisema kwa sasa hawezi kutoa idadi ya wanachama ambao wamechukua fomu ya kuwania nafasi hiyo hadi siku ya mwisho ambayo ni Julai 10, mwaka huu.

**TARIME**

Wanachama 15 wamechukua fomu za kuwania nafasi ya uenyekiti wa chama hicho ngazi ya wilaya kati yao watano ni wanawake.

Katibu wa CCM Wilaya ya Tarime, Valentine Maganga, alisema wanachama zaidi ya 50 wamejitokeza kuchukua fomu katika nafasi mbalimbali, huku akiwataja kuwa ni Marwa Daud Ngicho, anayetetea nafasi hiyo.

Mwingine ni Bwire Alliance, Jackson Mwera, Godfrey Francis, Peter Babere, Maseke Mohoni, Silvanus Paul Mosore na Anet Peter ambaye ni mwanamke peke kwenye nafasi hiyo.

Naye Katibu wa UWT Wilaya ya Tarime, Mwanaid Mbishu, alisema waliochukua fomu za kuwania uenyekiti ni Joice William anayetetea nafasi hiyo, Veronika Merengo, Martina Waisaka na Monika Mwenge.

Kwa upande wa nafasi ya Uenyekiti Jumuiya ya Wazazi Wilaya Tarime, waliochukua fomu ni pamoja na Mwikwabe Mangaraya anayetetea nafasi yake, Laurent Nyablangeti na Christopher Onditi.

**■Imeandikwa na Marco Maduhu (SHINYANGA) na Samson Chacha (TARIME)**


## JODAC PROFESSIONAL LIMITED NA TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO. LIMITED
## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **JODAC PROFESSIONAL LIMITED** na **TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO. LIMITED** Kwa Idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED** tunatoa muda wa siku 14 wadaiwa waliorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **MWANGAHAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED**, Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Mnada utafanyika Mahali dhamana ilipo kama ifuatavyo;

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SAKINA S. KIGOLA | SAKINA SALEHE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIMARA GOLANI UBUNGO, DAR ES SALAAM | 21-07-2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | JODAC PROFESSIONAL LIMITED |
| 2 | ABDALLLAH HASSAN JUMA | ABDALLLAH HASSAN JUMA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA; TMK045157 na TMK045156 | CHARAMBE RANGITATU, TEMEKE, DAR ES SALAAM | 22-07-2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | JODAC PROFESSIONAL LIMITED |
| 3 | EMILY D. MAARIFA | BEATUS SHATIEL MANGA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA; TMK032472 | MGAGALA KUU, KIZUIANI, TEMEKE, DAR ES SALAAM | 25-07-2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | JODAC PROFESSIONAL LIMITED |
| 4 | RICHARD S. SEGANJE | RICHARD S. SEGANJE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA; ILA017682 | UKONGA MWEMBE MADAFU, ILALA, DAR ES SALAAM | 26-07-2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | JODAC PROFESSIONAL LIMITED |
| 5 | YAHAYA YUSUPH KESEKE | YAHAYA YUSUPH KESEKE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA; TMK044735 | KEKO, MWANGA B, TEMEKE, DAR ES SALAAM | 27-07-2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | JODAC PROFESSIONAL LIMITED |
| 6 | SIMON MWAVIPA MANGASIN | SIMON MWAVIPA MANGASIN | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA; ILA028517 | KITUNDA, MWANAGATI, ILALA, DAR ES SALAAM | 28-07-2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | JODAC PROFESSIONAL LIMITED |
| 7 | SIMON MWAVIPA MANGASIN | SIMON MWAVIPA MANGASIN | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MACHIMBO KIPUNGUNI, ILALA, DAR ES SALAAM | 28-07-2022 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA | JODAC PROFESSIONAL LIMITED |
| 8 | COSMAS BRIAN MUSHI | COSMAS BRIAN MUSHI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBEZI MSUMI, UBUNGO, DAR ES SALAAM | 29-07-2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | JODAC PROFESSIONAL LIMITED |
| 9 | ABELL YESAYA SHEMKONGWA | ABELL YESAYA SHEMKONGWA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | JOGOO, MBEZI JUU, DAR ES SALAAM | 29-07-2022 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA | TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO. LTD |
| 10 | TERESIA ERICK SHAYO | THERESIA ELIKI SHAYO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MPONDA, MBAGALA, DAR ES SALAAM | 30-07-2022 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA | TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO. LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya Tangazo hili
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo
3. Mshindi anatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana ilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA**

| MANAGING DIRECTOR<br>TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO. LTD<br>P.O.Box 71418<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0692 926969/ 0713 237650/ 0719 351040 | MANAGING DIRECTOR<br>JODAC COMPANY LIMITED<br>P.O.Box 12744<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0717 003423/ 0767 163637 | MANAGING DIRECTOR<br>MWANGA HAKIKA BANK MICROFINANCE BANK<br>S.L.P 11735<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0747666511 |
|---|---|---|

216935002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Shule za kata zimeonyesha nuru ya mafanikio ya elimu

**BARAZA** la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), juzi lilitangaza matokeo ya mitihani ya kidato cha sita iliyofanyika Mei, mwaka huu. Matokeo hayo , yameonyesha kuwa ufaulu wa jumla umeongezeka hadi kufikia asilimia 99.97 kulinganisha na asilimia 99.03 ya matokeo ya mwaka jana.

Licha ya kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu, matokeo ya mwaka huu yametoa taswira nyingine baada ya shule mbili za kata kuwa katika orodha ya 10 bora na kuzibwaga shule kongwe za serikali na zile maarufu zinazomilikiwa na taasisi na watu binafsi.

Shule hizo, Mkindi ya Tanga na Ziba ya Tabora zimeshika nafasi ya tisa na ya 10 mtawalia zikiungana na Kemes (Kagera), Kisimiri (Arusha), Tabora Wavulana, AHMES (Pwani), Dareda (Manyara), Nyaishozi (Kagera) na Mzumbe ya Morogoro.

Hatua ya shule hizo kuchomoza katika nafasi 10 bora, ni ishara kwamba kumekuwa na maendeleo makubwa kitaaluma katika shule zilizoanzishwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) ulioasisiwa mwaka 2006. Kuasisiwa kwa mpango huo uliolenga kila kata kuwa na angalau shule moja ya sekondari, kulitokana na ongezeko la ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba kutokana na mafanikio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM).

Matokeo ya kwanza ya mitihani yaliyohusisha shule za MMES, maarufu kama shule za kata, yalionyesha shule nyingi kuburuza mkia na Watanzania wengi kubeza kwamba zilianzishwa kwa mtindo wa zimamoto. Baadhi ya wadau walidai kuwa kufeli kwa maelfu ya wanafunzi katika shule hizo, kulitokana na sababu mbalimbali zikiwamo uhaba wa miundombinu, ukosefu wa vitabu vya ziada na kiada, uhaba wa walimu, nyumba za walimu na hosteli.

Kutokana na matokeo hayo duni, serikali iliafiki kasoro hizo na kuweka mkazo katika kuzirekebisha kwa kuajiri walimu kila mwaka, kujenga vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, maabara za masomo ya sayansi, nyumba za walimu na hosteli. Kero hizo zimekuwa zikipungua kila mwaka na hatimaye kiwango cha ufaulu kuanza kupanda mwaka hadi mwaka.

Kuibuka kwa shule hizo katika shule 10 bora ni dhahiri kwamba kiwango cha elimu katika shule zilizokuwa zikionekana hazina ubora, kumebadili fikra na mawazo yaliyokuwa yametawala, hivyo kuwa tishio kwa shule kongwe na maarufu zilizokuwa zikitamba mara kwa mara kila matokeo ya mitihani ya kidato cha nne na cha sita yalipokuwa yanatangazwa.


Kwa hakika Mkindi na Ziba, ambazo ziko katika mazingira ya vijijini, zimeonyesha mfano na kuudhihirishia umma kwamba mpango wa serikali kuwa na shule katika kila kata ulikuwa na malengo mazuri ya muda mrefu katika maendeleo ya elimu.

Pia shule hizo zimedhihirisha kauli ya mara kwa mara ya serikali kwamba shule za kata miaka michache ijayo zitakuwa kimbilio kwa vijana wengi na hata kwa Watanzania waliokuwa na kasumba ya kuamini kwamba elimu nzuri inapatikana kwenye shule zinazomilikiwa na mashirika ya dini, taasisi na watu binafsi.

Kutokana na shule hizo kuibuka kidedea, ni nafasi ya shule zingine za kata kujifunza ni mbinu gani zilizotumika katika kuziwezesha kushika nafasi za juu za ufaulu ili kuongeza idadi ya shule za kundi hilo katika kupandisha kiwango cha ufaulu.

Pamoja na hayo, kama wahenga wasemavyo mgema akisifiwa tembo hulitia maji, walimu na wanafunzi wa shule hizo zilizobwaga shule kongwe, wasibweteke bali waongeze kasi na kuendelea kuwa katika kundi hilo pamoja na kuweka malengo ya kushika nafasi za juu zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tujitahidi kufikia asilimia 70 ya waliochanjwa UVIKO-19

Na Sabato Kasika

**TANZANIA** ilikuwa nyuma katika utoaji wa chanjo ya UVIKO-19, lakini sasa mwamko mkubwa umeongezeka kutoka asilimia 6.3 hadi kufikia asilimia 12.4 ya utoaji wa huduma hiyo kwa Watanzania.

Pamoja na jitihada hizo, bado lengo la serikali ni kuwa na asilimia 70 ya Watanzania waliochanjwa halijafikiwa tangu uzinduzi wa kampeni ya chanjo iliyofanyika mwishoni mwa Julai mwaka jana.

Inaelezwa walau hatua ambayo Tanzania imefikia sasa inatoa moyo, ingawa bado elimu zaidi inatakiwa kuendelea kutolewa kwa raia wajue umuhimu wa chanjo na hata wajitokeze kwa wingi kuchanjwa.

Ni suala hilo la elimu na uhamasishaji wa chanjo, vimemsukuma Katibu Mkuu Msaidizi na Mratibu Mkuu wa Kimataifa wa mapambano dhidi ya UVIKO-19 kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) , Ted Chaiban, kuja nchini na juzi alikuwa katika viwanja vya Mwembeyanga, Temeke, Dar es Salaam kuhamasisha chanjo.

Hapo akapongeza jinsi nchi inavyopambana na ugonjwa huo, hasa kutoka kiwango cha asilimia sita hadi kufikia asilimia 12.4 ya waliochanjwa.

Ninadhani pongezi hizo zingefaa kuwa chachu kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO-19, kwani hali inaonyesha kuwa watu bado wanasuasua.

Kwanini ziwe chachu? Ni kwa sababu Watanzania wako nyuma kufikia ile asilimia 70 iliyokusudiwa na serikali, pia ugonjwa huo hatari unaendelea kuenea katika maeneo mbalimbali duniani.

Hivyo, suala la kuendelea kuchukua tahadhari na kupata huduma ya chanjo ni jambo la msingi, ambalo kila Mtanzania anatakiwa kuchukulia kwa uzito zaidi, ili kuhakikisha afya yake inakuwa salama.

Kama nilivyoeleza kuwa lengo la serikali ni kuwa na asilimia 70 ya Watanzania waliochanja, ili kuwa na walau na kinga sahihi. Naamini kutofikia asilimia hiyo kumemfanya mgeni huyo kutoka WHO kuja kusaidia hamasa na amana kubwa kwetu sote.

Ikumbukwe, chanjo ilizinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa Julai mwaka jana na sasa tunaelekea kutimiza mwaka mmoja tangu huduma hiyo ianze kutolewa nchini.

Hapo kuna haja ya asilimia 12.4 ya waliochanjwa. Nadhani ipo haja kwa kila Mtanzania kutafakari na kisha kuchukua hatua zitakazomwezesha kujikinga na UVIKO-19, hasa kwa kuachana na elimu potofu.

Tangu ugonjwa huo nchini, kumekuwapo elimu nyingi zinazohusu afya zinazotolewa, hata na watu wasio na utaalamu wa afya, hali ambayo inawezekana wamechangia kukwamisha chanjo.

Lakini, yapo maeneo yaliyopiga hatua katika utoaji chanjo, mfano hai ni Mganga Mkuu wa Wilaya ya Temeke (DMO) Dk. Irene Haule, anayesema amefanikiwa kuvuka kiwango cha utoaji huduma ya chanjo elekezi, kutoka watu 3,500 hadi kufikia idadi ya wapata huduma 7,000 kwa siku.

Sababu kubwa ya kuvuka lengo, inaelezwa inatokana na mikakati waliojiwekea ikiwamo ya utoaji elimu kwa jamii, ambayo kwa sasa wana mabanda matano ndani ya viwanja vya Sabasaba.

Utaratibu mwingine, ni kwamba wanatoa huduma nyumba kwa nyumba na kwenye vituo valivyoteng-wa na huduma nyingine, huku chanjo ya UVIKO-19 ikipewa kipaumbele kuhakikisha wananchi wanakuwa salama kupitia kinga hiyo.

Mikakati ya utoaji huduma ya chanjo ya UVIKO-19 kwa njia kama elimu, imesaidia kuongeza idadi ya wanaopata huduma hiyo, ikiwa ni jitihada za kiserikali kuwalinda wananchi wake dhidi ya magonjwa.

Hatua zinazofanywa na Temeke nazisifu ni nzuri na ninaamini zikiigwa na maeneo mengine ya Dar es Salaam na hata nchi nzima kwa ujumla, lengo la serikali la kutaka asilimia 70 kupata huduma hiyo zitawezekana.

Jambo la kwanza ni kutambua kuwa ugonjwa huo upo, kisha kuchukuliwa hatua zinazoelekezwa na wataalamu wa afya na kuweka pembeni elimu ya mitaani, ambayo kimsingi inapotosha.

Iwapo kila mmoja wetu atajua na kutekeleza wajibu wake dhidi ya UVIKO-19, ni wazi asilimia ya waliochanjwa inaweza kuongezeka hadi kufikia lengo au kulivuka na hivyo kujiweka katika mazingira salama zaidi.

# Waonywa kumaliza kesi ukatili nyumbani

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI wametakiwa kuacha mchezo wa kumaliza kesi katika ngazi ya familia, kwa kuwa inasababisha madhara makubwa kwa wahusika waliotendewa ukatili.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Baraka Lucas katika maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITE) katika viwanja vya Sabasaba.

Lucas alisema kuna kesi zinazomazilika kirafiki ama katika ngazi ya jamii, hasa katika matendo ya ukatili jambo ambalo sio sahihi.

"Kimsingi mtu yeyote hata kama ni ndugu yako ama jirani ametenda kosa, hilo ni kosa kinachovunjwa pale ni sheria na haki ya mtu weka urafiki mbali na undugu angalia haki ya mtu," alisema Lucas.

Alisema jamii inapotokea imebaini tatizo hilo ni vyema ikawasilisha taarifa rasmi kwenye mamlaka husussani Jeshi la Polisi, vituo vya afya na mamlaka za sheria, ikiwamo mahakama ili mashauri hayo yaweze kusikilizwa.

"Kumaliza kesi hizo katika ngazi ya familia kuna athari kubwa kwa mtendewa wa kosa na kwa mtenda kosa. Mtendewa kosa anakwenda kuathirika anapoona yule aliyemfanyia tendo la ukatili bado yupo mtaani maana yake anaweza kupoteza amani ama kujidhuru ama akaenda kumdhuru aliyemtendea ubaya," alisema.

Aidha, kuongezeka kwa vitendo vya ukatili ni matokeo ya ufanisi wa mfumo uliowekwa na serikali ambao umesaidia upatikanaji wa taarifa ya matukio hayo.

Alisema jukumu la kulea watoto, kulinda wazee, kulinda kundi la vijana ni la jamii yote kwa ujumla wanaamini kuwa ulinzi na usalama wa binadamu unapatikana kwa sehemu kubwa katika jamii.

Lucas alisema kwa sasa watu hawawajibiki kusimamia wengine ambao hawawahusu. "Sasa hivi wanasema mtoto wa mwenzako mkubwa mwenzio hicho ni kitu kibaya kinaharibu mifumo ya jamii ndiyo maana zamani mtu aliweza kutoa adhabu kwa mtu ambaye sio ndugu yake anapokwenda kinyume na watu wakikubaliana na hilo ila kwa sasa hauwezi kumpiga mtoto wa mtu," alisema.

# Anayeshtakiwa kukutwa na nyeti za kike 5 adaiwa kuzipeleka Rufiji

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Maswa, Salum Nkonja (23), anayetuhumiwa kukutwa na sehemu za siri tano za mwanamke na chuchu tano wakati anahojiwa, amedai alitumwa kuvirudisha viungo hivyo kwa mtu mmoja anayekaa Rufiji.

Wakili wa Serikali, Adolf Verandumi, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalira wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, alidai hayo jana alipomsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Alidai kuwa wakati wa mahojiano, mshtakiwa aliwaambia polisi kuwa vitu hivyo alitumwa kuvirudisha kwa mtu mmoja anayekaa Rufiji.

Wakili Verandumi alidai kuwa Oktoba 29, 2017, mshtakiwa alisafiri kutoka Kahama kwenda Dar es Salaam kwa kutumia usafiri wa basi aina ya RedBelt, ambapo Oktoba 30, 2017 alifika katika kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani cha Ubungo.

Alidai maofisa walipata taarifa ya kuwapo kwa mtu anayeuza viungo vya binadamu na hivyo kukamatwa na nyara za serikali na viungo vya binadamu.

Mshtakiwa anadaiwa kukutwa na viungo vya binadamu ambavyo ni sehemu za siri tano za mwanamke, mafuvu mawili ya binadamu na chuchu tano za wanawake.

Alidai baada ya kukamatwa, vitu hivyo viliorodheshwa katika hati ya ukamataji na mshtakiwa kutia siani na kisha kupelekwa kituo kikuu cha polisi kilichoko jijini kwa ajili ya mahojiano.

Wakili huyo alidai kuwa Novemba 2, 2017, askari polisi pamoja na mshtakiwa waliongozana hadi Kituo cha Polisi cha Chumbi kilichoko Kijiji cha Khanga wilayani Rufiji mkoani Pwani kwa mtu aliyemtaja kwa jina la Samuel Rwiza lakini hawakumpata mtu huyo.

Alidai kuwa Novemba 5, 2017, askari polisi walikwenda Kagongwa wilayani Kahama, nyumbani kwa mshtakiwa ambapo walimkuta mama wa mshtakiwa na kuwathibitishia kuwa Salum ni mwanawe na amemaliza kidato cha nne hivi karibuni.

Alidai kuwa viungo hivyo vya binadamu vilipelekwa kwa Mkemia Kuu wa Serikali kwa ajili kuvipima huku nyara za serikali zilizokamatwa zikipelekwa kwa Ofisa Wanyamapori kwa ajili ya kuthibitisha na baada ya hapo mshtakiwa alifikishwa mahakamani.

Mshtakiwa baada ya kusomewa maelezo yake, alikubali maelezo yake binafsi na kwamba alisafiri kwenda Dar es Salaam, huku maelezo mengine akikana.

Hakimu Rugemalira baada ya kusikiliza maelezo hayo, aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 19, 2022 ambapo upande wa mashtaka wataanza kutoa ushahidi.

Katika kesi ya msingi, mshtakiwa anadaiwa kutenda makosa yao kati ya Oktoba 30, 2017 na Novemba 2017 katika eneo la Ubungo, Wilaya ya Ubungo, ambapo alikutwa na vitu hivyo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kusherehekea miaka 20 ya mafanikio ya benki hiyo uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Uendeshaji, Nelson Swai, Mkurugenzi wa Mikopo, Isidori Msaki, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Rahma Ngassa na Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa benki hiyo, Ester Bgoya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachumi wafunguka kupanda bei ya mafuta

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kutangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli, huku kukiwa na afueni kidogo kwa watumiaji dizeli, wachumi wafunguka kisababishi cha hali hiyo.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, wachumi hao walisema serikali ilichokifanya ni kupunguza makali kwa wananchi kwa sababu bei ya mafuta duniani bado ipo juu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini Tanzania (REPOA), Dk. Donald Mmari, alisema serikali ilichokifanya ni kuweka uwiano kati ya petroli na dizeli ambayo inaonekana imeshuka.

"Ninachokiona wamefanya uwiano kidogo kwa kupunguza dizeli kidogo ambayo ndiyo inatumika zaidi kwenye uzalishaji viwandani, usafiri na uchukuzi," alisema.

Mchumi huyo alisema bei ya mafuta duniani imepanda kutokana na uhaba uliopo sasa unaosababishwa na vita na mahitaji kuongezeka baada ya uchumi kufunguka.

"Bahati mbaya vita vya Ukraine na Urusi vimefanya mafuta kupungua kwenye soko na bei kuendelea kupanda, kwa hiyo kama serikali isingeingilia kati hili kwa kuweka fedha, bei ingepanda zaidi," alisema.

Dk. Mmari alisema kiasi cha fedha ambacho serikali imekiweka kwenye mafuta kimepunguza makali.

"Serikali haiwezi kupunguza kabisa wakati bei duniani inapanda, maana yake upunguze matumizi ya bajeti ambapo itakufanya ushindwe kutoa huduma nyingine za msingi kwenye sekta ya afya na miundombinu.

"Serikali inajitahidi nadhani hata hiyo bei ilivyopanda kidogo haina maana kwamba bei kwenye soko la dunia imepanda kidogo, imepanda zaidi lakini serikali imeamua kupunguza kidogo, hata Norway inayozalisha mafuta niliangalia jana bei zake za mafuta zimepanda na wanayazalisha wala hawayasafirishi," alisema.

Mtaalamu wa Uchumi, Dk. Donath Olomi, alisema kupanda kwa bei ya nishati hiyo siyo habari njema kwa kuwa itafanya mfumuko wa bei za bidhaa kutokana na gharama za uzalishaji kuongezeka na kusababisha maisha ya watu kuwa magumu.

Aliongeza kuwa bidhaa zikipanda zitasababisha makusanyo ya kodi kushuka kwa sababu wafanyabiashara watalazimika kupandisha bei ya bidhaa huku watumiaji wakishishindwa kuzinunua.

"Ukiwa unafanya biashara, kodi ya mapato inalipa asilimia ya faida, kwa hiyo gharama zikiongezeka faida inapungua, faida ikipungua na kodi ya mapato inapungua, kwa kweli hii inaathiri watu wengi kuanzia msafirishaji hadi mnunuaji," alifafanua.

Mchumi Dk. Haji Semboja alisema kupungua kwa bei ya mafuta ni jambo ambalo haliwezekani kwa sasa.

Alisema lingewezekana kama uzalishaji wa gesi ungekuwa umeongezeka, hivyo wakati wa uhaba wa mafuta duniani, nchi ingetumia gesi kupunguza makali kwa wananchi.

Juzi, EWURA ilitangaza bei kikomo ambazo zimeanza kutumika kuanzia jana.

Taarifa ya mamlaka hiyo ilisema katika kukabiliana na ongezeko la bei za mafuta, serikali imetoa ruzuku nyingine ya Sh. bilioni 100 kwa mwezi Julai na imeelekezwa katika mafuta ya petroli na dizeli.

"Kiasi kikubwa cha ruzuku kimeelekezwa katika mafuta ya dizeli kwa lengo la kudhibiti mfumuko kwa bei kwa sababu dizeli hutumika zaidi katika shughuli za kiuchumi ikiwamo katika uzalishaji viwandani na katika usafirishaji wa mazao na bidhaa nyingine," ilifafanua mamlaka hiyo katika taarifa yake ya juzi usiku.

Ilisema ruzuku ya Sh. bilioni 100 imesaidia kupunguza bei ya mafuta kwa mwezi Julai ambapo kwa Mkoa wa Dar es Salaam bei ya petroli kabla ya ruzuku ilikuwa Sh. 3,497 na baada imekuwa ni Sh. 3, 220.

# Waandishi wataja vifungu kufutwa Sheria ya Habari

**Na Mary Geofrey**

WAANDISHI wa habari nchini wametaka kufutwa kwa vifungu vya 35, 36, 50 (1)(a)(ii) vya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 kwa sababu vinaeleza kosa la kashfa ni jinai badala ya madai.

Waandishi wa habari waliwasilisha kilio chao hicho jijini Dar es Salaam juzi, wakisisitiza kuwa vifungu hivyo vinalenga kukomoa wanahabari.

Mhariri wa Gazeti la Tanzania Daima, Maregesi Paul, alisema vipengele hivyo vinalenga kukomoa wanahabari kwa kuwa uzito wake ni mkubwa tofauti na kosa la kashfa.

"Kosa la kashfa halina uzito mkubwa kama linapogeuzwa kuwa jinai na walipoliweka hilo walitaka kukomoa. Sasa hapo mwandishi anachukuliwa kama mhujumu uchumi, hii ni hatari sana," alisema Maregesi.

Mwandishi wa Habari wa Mwanahalisi Digital, Regina Mkonde, alisema kosa la kashfa kugeuzwa jinai kunamweka mwandishi wa habari katika hatari zaidi na kumjaza hofu.

Makamu Mwenyekiti wa MISA-TAN, Wakili James Marenga, akitolea ufafanuzi vifungu hivyo vya sheria, alisema hatua ya kosa la kashfa kugeuzwa jinai, inaongeza hofu na sintofahamu kwa wanahabari nchini.

"Tunapendekeza kuwa mashauri yote yatakayotokana na kashfa yaendeshwe kama kesi za madai siyo jinai," alisema Marenga.

Alisema madhumuni ni kuhakikisha vikwazo katika uhuru wa habari na uhuru wa kujieleza vinaondolewa.

Wakili huyo wa kujitegemea alieleza zaidi kuwa kugeuza kashfa kuwa ya jinai kunaleta hofu na kufifisha haki ya kujieleza na kutoa maoni.

"Kifungu cha 37 kinasema kwamba, uchapishaji wa kashfa ni kosa la jinai isipokuwa kama jambo lililochapishwa ni la kweli na limechapishwa kwa manufaa ya umma; pia kama uchapishaji huo umetolewa kama upendeleo wa kutoshtakiwa (privileged) kwa kashfa na ulikuwa ni manufaa kwa umma," alisisitiza.

Alisema kama uchapishaji huo umetolewa kama upendeleo wa kutoshtakiwa (privileged) kwa kashfa na ulikuwa ni manufaa kwa umma, kifungu hicho cha sheria hakijaweka vigezo vingine vinavyoonyesha kuwa uchapishaji wa kashfa siyo kosa la jinai.




Meneja Mauzo wa bidhaa za Intanet Tigo, Edwin Mgoa (kushoto), na Meneja Uhusiano wa Infinix Tanzania, Eric Mkomoye, wakionyesha simu janja aina ya Infinix Note 12 VIP, wakati wakiitambulisha katika maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaleta neema wabunifu TEHAMA

**Na Frank Monyo**

WABUNIFU katika tasnia ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), sasa wataweza kutumia rasilimali adimu za mawasiliano zikiwamo namba fupi, masafa na kikoa cha.tz ili kukamilisha ubunifu wao.

Hatua hiyo ni baada ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuingia makubaliano ya ushirikiano wa ubadilishanaji rasilimali hizo na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), ambayo itapewa rasilimali hizo kwa niaba ya wabunifu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alibainisha hayo kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere kwenye maonesho ya viwanda na biashara ya Sabasaba alipotembelea banda la TCRA.

"TCRA imejipanga vilivyo kuhakikisha wabunifu na wanafunzi ambao wana mawazo mazuri ya kuendeleza Uchumi wa Kidijitali, tunawawezesha," alisema, Dk. Jabiri na kuongeza;

"Ushirikiano baina ya taasisi hizo mbili unalenga kuwapatia wigo mpana zaidi wa ubunifu, vijana wanaoshiriki kuleta mawazo mapya katika TEHAMA na kwamba kupitia COSTECH, Mamlaka ya Mawasiliano itawapatia majukwaa na raslimali adimu za majaribio," alisema.

"Tuna rasilimali namba, rasilimali masafa na dot tz; ambavyo kwa mujibu wa taratibu siku za nyuma ulikuwa unaweza kupata rasilimali hizi kwa kulipa leseni, kwa sasa kama wewe ni 'start-up' (mbunifu) basi utapata bila gharama na hiyo ndiyo sababu tumetengeneza ushirikiano na wenzetu wa COSTECH," aliongeza.

Dk. Jabiri alisema katika kuhakikisha mpango unafanikiwa TCRA pia imekubaliana na Tume ya TEHAMA kuwajengea uwezo wabunifu hasa vijana, ili kuhakikisha wanatoa ushiriki wenye tija katika ukuzaji uchumi wa kidijitali.

Pia, alisema katika kuhakikisha azma hiyo inafanikiwa TCRA imeipatia jengo la ofisi Tume hiyo, ili kuiwezesha kutekeleza malengo hayo ikiwamo kuimarisha mazingira na miundombinu itakayowasaidia wabunifu katika TEHAMA.

Alibainisha kuwa hatua hiyo inalenga kukuza ajira, kuwezesha upatikanaji wa bidhaa na huduma bila vikwazo vingi miongoni mwa faida za kuwajengea uwezo vijana wabunifu wa TEHAMA.

Aliongeza kuwa mamlaka hiyo kwa sasa inajikita kuwajengea uwezo vijana kuanzia shule ya msingi, ambako tayari mamlaka inawezesha uanzishwaji wa klabu za kidijitali ili kukuza kizazi cha vijana wanaoiishi TEHAMA kwa vitendo.

Katika hatua nyingine, Dk. Jabiri alisisitiza kuwa mamlaka anayoisimamia itaendelea kusimamia ubora wa vifaa vya mawasiliano ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za mawasiliano kutoka kwenye vifaa vyenye ubora.

"Sisi ni 'facilitators' (wawezeshaji) kwa hiyo unapokuja na uwekezaji mpya unaohusiana na mawasiliano au vifaa vitakavyowezesha muendelezo wa mnyororo wa mawasiliano tupo pale kufanya tathmini ya ubora wa kifaa hicho, kiwe kimetengenezwa nchini au nje," alibainisha Jabiri na kuongeza:

Alibainisha kuwa hadi sasa vifaa vya mawasiliano ya kiganjani vyenye uwezo wa kutumia intaneti katika teknolojia za 3G na 4G ni asilimia 28 pekee, akibainisha kuwa ikiwa uwekezaji wa utengenezaji vifaa vya mawasiliano hapa nchini utapatikana upo uwezekano mkubwa idadi ya watumiaji wa mtandao kuongezeka kutoka asilimia 28 za sasa.

# Mkurugenzi Lake Oil apewa tuzo Uingereza

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Lake Oil Group, Ally Edha Awadh, ametunukiwa Tuzo ya Mfanyabiashara Kijana kwa Mwaka 2022 kwa Afrika.

Alipokea tuzo hiyo juzi London, Uingereza baada ya kuwashinda wapinzani wake watatu, Sangu Delle, Mwenyekiti wa Kampuni ya Golden Palm Investments Corporation ya Ghana; Stephen Sembuya, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Pink Foods Industries ya Uganda; na Emmanuel Ademola Ayilara, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya LandWey Investment Limited ya Nigeria.

Awadh ambaye ni Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo iliyojikita kwenye biashara ya mafuta na gesi, alipokea tuzo hiyo kwenye Ukumbi wa House of Lords jijini London, Uingereza ambazo ni miongoni mwa kumbi maarufu zaidi duniani. Tuzo hizo zinazotolewa na Jarida la African Leadership.

Lake Oil imejikita zaidi katika biashara ya vituo vya kuuza mafuta kwenye maeneo mbalimbali nchini sambamba na gesi inayotumika majumbani.

Mbali na hilo, Awadh anatajwa kama mfano kwa vijana ambapo kupitia kampuni zake hizo, amesaidia kutoa ajira kwa makundi ya vijana huku ufanisi wa kampuni hizo ukichukuliwa kama mfano bora kwa vijana kuendesha biashara kwa tija.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji huyo wa Lake Oil alisema ilikuwa kumbukumbu ambayo hataisahau kwa maisha yake yote.

"Nilikabidhiwa Tuzo ya Kiongozi wa Biashara Vijana barani Afrika katika Jumba la Mabwana Mashuhuri hapa London, mbali ya kuwa faraja kwangu, pia nimefurahi zaidi tuzo hii kupatikana kwa kijana wa Kitanzania," alisema Awadh.

"Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa mama na baba yangu kwa sala na baraka zao zisizo na mwisho, familia yangu, haswa mke wangu, kwa nyakati zote ambazo nimekuwa mbali na kuzingatia biashara zetu," alisema Awadhi.

Pia alitoa shukrani kwa timu nzima ya wafanyakazi wa kampuni za Lake Oil sehemu mbalimbali Afrika, akimshukuru Mungu kwa kuwapa nguvu za kufanya kazi na kutimiza malengo yao.

## Serikali kuwawezesha wavuvi vifaa vya kisasa

**Na Mbaraka Kambona,** PWANI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali imejipanga kuwawezesha wavuvi vifaa vya kisasa ikiwamo boti kuvua samaki kwenye kina kirefu ili waongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo, kuinua uchumi wao na kukuza Pato la Taifa.

Ndaki alibainisha hiyo wakati wa hafla fupi ya kuzindua na kukabidhi jengo jipya kwa Kikundi Shirikishi cha Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi cha Dunda (BMU) kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa rasilimali za bahari katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi iliyofanyika wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani, Julai 5, 2022.

Alisema serikali inataka kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi na ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan ameongeza bajeti ya Sekta ya Uvuvi ya mwaka 2022/2023 na sehemu yake itatumia kununua boti zaidi ya 300 ili wakopeshwe wavuvi na kuboresha shughuli zao.

Pia boti hizo zitasaidia wavuvi kwenda katika kina kirefu na kuvuna mazao mengi ya samaki na kufanya viwanda vya kuchakata samaki kufanya kazi kwa uwezo wake tofauti na ilivyo sasa viwanda vingi vinafanya kazi chini ya uwezo uliosimikwa.

Waziri Ndaki aliwataka wananchi kuunga mkono juhudi za serikali kupiga vita uvuvi haramu huku akisisitiza kuwa kazi hiyo sio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi pekee bali ni ya kila mmoja.

"Samaki ni lishe, samaki ni pesa, samaki ni biashara na samaki ni ajira, tushirikiane kupiga vita uvuvi haramu," alisema.

Aliwataka viongozi wa Vikundi Shirikishi vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi kuwa waadilifu na kujiepusha na vitendo vya rushwa na upendeleo kwa kuwa ndiyo chanzo cha uvuvi haramu.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Abdallah, aliishukuru serikali ilivyojipanga kuwawezesha wavuvi akiamini kuwa kwa mipango hiyo wavuvi katika wilaya yake watanufaika kupitia shughuli zao hizo.

**"Samaki ni lishe, samaki ni pesa, samaki ni biashara na samaki ni ajira, tushirikiane kupiga vita uvuvi haramu," alisema.**

# TAWIRI yaeleza umuhimu wa kutunza shoroba

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), imesema migogoro kati ya binadamu na wanyamapori inatokana na shughuli za kibinadamu kuvamia katika maeneo ya asili ya mapito ya wanyamapori maarufu kama shoroba.

Imesema ili migogoro hiyo iweze kumalizika ni muhimu serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na vyombo vya habari, ikaweka nguvu za pamoja ikiwamo kuelimisha jamii umuhimu wake kuhakikisha wananchi wanaelewa umuhimu wa maeneo hayo.

Mtafiti Mkuu kutoka TAWIRI, Dk. Stephen Nindi, alisema hayo wakati akiwasilisha mada ya Jukumu la Serikali katika kulinda shoraba kwenye mafunzo yaliyotolewa kwa njia ya mtandao kwa waandishi wa habari wa uhifadhi kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Mafunzo hayo yametolewa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kupitia mradi wa Tuhifadhi Maliasili unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Marekani (USAID).

Dk. Nindi alisema kwa sasa Tanzania ina jumla ya shoroba 52 na kati ya hizo 42 zimepitiwa na kufanyiwa kazi, lakini wamebaini nyingi za asili zimevamiwa na jamii na kuleta athari kwa viumbe hai.

Alisema uvamizi huo umetokana na asilimia 90 ya shoroba zote zimepitia katika ardhi ya vijiji hivyo kutokana na mabadiliko ya tabianchi wananchi wamevamia maeneo yaliyohifadhiwa, ikiwamo mapito na mazalio ya wanyama maarufu kama shoroba.

"Shoroba nyingi zipo katika ardhi za vijiji na wananchi wamezivamia kufanya kilimo na ufugaji pamoja na makazi baada ya kutokea mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yao sasa serikali na wadau wa sekta binafsi, ikiwamo nyie waandishi wa habari lazima tutoe elimu kwa wananchi umuhimu wake katika kuhifadhi maliasili zetu na viumbe hai," alisema Dk. Nindi.

Alisema shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo, ufugaji na ujenzi wa makazi wanyama ambao wamezoa kupita katika maeneo yao wanakutana na mazao ya wakulima na kula hali inayosababisha migogoro hiyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Utafiti wa Tume ya Taifa Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi (NLUPC), Dk. Joseph Layson, alisema ni wadau wakubwa wa uhifadhi ndiyo maana katika mpango wao wa matumizi bora ya ardhi wameanza kutenganisha eneo la uhifadhi na makazi ya watu kulinda.

Alisema wilaya 42 zimeandaliwa matumizi bora ya ardhi huku maeneo ya uhifadhi na vyanzo vya maji yakitenganishwa kwa ajili ya kuyalinda na kuhifadhi kwa manufaa ya kutunza rasilimali zilizopo.



Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Abdallah (kushoto), akimweleza jambo Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, katika hafla fupi ya kuzindua na kukabidhi jengo jipya kwa Kikundi cha Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi cha Dunda (BMU) iliyofanyika wilayani Bagamoyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama kuendesha mashauri saa 24

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Tanzania kupitia Kituo Jumuishi cha Masuala ya Familia kilichoko Temeke, jijini Dar es Salaam, ina mpango wa kuendesha mashauri saa 24 ili wafanyakazi waendelee na majukumu yao muda wa kazi.

Hayo yamesemwa jana na Mkuu wa Kitengo cha Maboresho ya Mahakama, Dk. Angelo Rumisha, wakati Benki ya Dunia ilipotembelea banda la mahakama katika maonyesho ya 46 ya Sabasaba, Dar es Salaam.

Dk. Rumisha alisema baada ya kuwapo kwa kituo hicho kimepokea kesi nyingi, namna ya uendeshaji wa mashauri hayo umekuwa na changamoto mbalimbali, ndiyo maana ya kutaka kuanzisha mpango huo.

"Kituo hiki ni cha kipekee Afrika na cha pili ulimwenguni baada ya Singapore, vituo ambavyo vinashughulikia mashauri ya kifamilia ikiwamo ndoa, mirathi na talaka, ndiyo maana mashauri ni mengi," alisema Dk. Rumisha.

Alisema wamepata changamoto ya watu kutaka huduma na kuwahudumia imekuwa changamoto, wamefikiria kufanya kazi saa 24 ili mtu mwenye shauri lake na ni mfanyakazi aende kazini halafu saa 11 au 12 jioni aende mahakamani kusikiliza shauri lake.

"Shauri hilo linaweza kuendeshwa hadi saa mbili asubuhi, aendelee na majukumu yake kama kawaida haya ndiyo maboresho tunayoyazungumzia ya Mahakama," alisema Dk. Rumisha.

Alisema mahakama hiyo kwa kushirikiana na Benki ya Dunia wanafanya huduma za uboreshaji wa mahakama katika utoaji haki tangu mwaka 2016.

Hata hivyo, Dk. Rumisha alisema baada ya miaka mitano ya ushirikiano wao na kutokana na mafanikio makubwa ambayo mahakama iliyopata katika uboreshaji wa huduma hizo, waliongeza fedha na muda hadi 2025 huku ikizingatia katika uwekaji wa miundombinu muhimu ya kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wote.

Alisema wanazingatia matumizi ya teknolojia katika utoaji wa haki na namna ya kubadili fikra katika masuala yote ya haki, kupunguza mashauri bila gharama za kesi ikiwamo umbali wa kufuata mahakama uboreshaji utakuwa haujafanyika.

Kwa upande wake, Kiongozi wa Timu ya ujumbe wa Benki ya Dunia, Christine Owuor, alisema katika miradi ambayo wameshaipitia, Tanzania imefanya vizuri na nyingine zinatakiwa kuiga jinsi ya kuboresha utoaji wa huduma za mahakama kwa wananchi.

Alisema wamewasili Tanzania kukagua utekelezaji miradi yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 65 (Sh. bilioni 141) kwa ajili ya uboreshaji wa utoaji wa huduma kwa mahakama.

# Wastaafu wafurahishwa VETA ubunifu kwa wanafunzi

**Habari zote na Elizabeth Zaya**

WASTAAFU wa Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), wamesema wanafurahishwa na juhudi zinazofanywa na mamlaka hiyo kwa kuendelea kuboresha mafunzo na kutoa wanafunzi bora ambao wanabuni vitu vinavyokidhi soko la sasa la mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Wakizungumza walipotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa (DITF), wastaafu hao walisema inatia moyo kuona VETA inavyobadilika kila mwaka.

"Kwa ujumla tumefurahia sana maonyesho, kuona vitu mbalimbali na jitihada za ubunifu ambazo zimefanyika ambazo zinaambatanisha kazi zilizofanywa na wanafunzi, tumeona kuna jitihada kubwa ya kupeleka nchi yetu mbele zaidi," alisema mmoja wa wastaafu hao Stephen Lazaro.

"Ukiangalia VETA kila siku kuna mabadiliko, inaendelea kukua, hata ukiangalia idadi ya washiriki kwenye banda hili imeongezeka sana na kazi zao ni nzuri zaidi na kuna upanuzi mkubwa wa teknolojia inayotumika katika mafunzo, kwa hiyo kwa ujumla imepata mafanikio makubwa zaidi."

Alisema ubunifu unaofanywa na VETA unaendelea kuiweka vizuri katika kutoa wanafunzi ambao wamebobea kwenye mahitaji ya viwanda.

"Kwa hiyo naamini wameona fursa iliyopo kwenye sekta ya viwanda na ndiyo maana wanafanya jitihada zaidi za kuboresha na kubuni teknolojia mpya kila siku," alisema Lazaro.

Alitoa wito kwa vijana pamoja na jamii kwa ujumla kuendelea kuiamini Mamlaka hiyo pamoja na vyuo vyake na kwenda kujifunza mambo mbalimbali na kufanya vitu ambavyo vitawasaidia kwenye kujiajiri.

"Huu ni wakati muafaka sasa kwa vijana waitumie VETA kwenda kupata stadi mbalimbali, kwa sababu tunaona kwa sasa namna ambavyo inapambana kwenda na mabadiliko ya teknolojia na kuja na vitu vya kisasa," alisema Lazaro.




Meneja Mwandamizi Idara ya Mikopo wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Joanitha Deogratias (wapili kushoto), akizungumza na baadhi ya wateja waliotembelea banda la benki hiyo katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa Sabasaba yanayofanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam. Wengine pichani ni maofisa wa benki hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtafiti agundua mbadala malisho wanyamapori

MTAFITI Mwandamizi wa Taasisi ya Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Dk. Jerome Kimaro, amegundua njia mbadala ya kuboresha malisho ya wanyamapori inayojulikana kitaalamu kama RangelandsCARE Project, ya kupunguza mimea vamizi katika Hifadhi ya Ngorongoro.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye banda la TAWIRI, Dk. Kimaro alisema pamoja na hifadhi hiyo ya Ngorongoro kuwa na umuhimu kitaifa na kimataifa kutokana na viumbe waliomo humo, vipo hatarini kupotea kutokana na kukumbwa na mimea vamizi kwa wingi.

Alisema hifadhi hiyo imekuwa ikikumbwa na changamoto ya mimea hiyo vamizi kwa kipindi cha miaka 10 sasa na kusababisha kupungua kwa ubora wa wanyamapori na baadhi ya mimea kupungua na kuhatarisha kutoweka kabisa.

"Kwa hiyo wadau wamekuwa wakijaribu kupambana na changamoto hii kwa miaka yote hiyo 10, na ndiyo maana sisi kama TAWIRI kupitia mimi, tukaamua kufanya utafiti na kuja na mbinu mbadala na madhubuti ambayo itasaidia kutatua mimea hiyo vamizi kwenye hifadhi yetu ambayo ina faida nyingi za kiuchumi, kiikolojia na kijamii," alisema Dk. Kimaro.

Alisema ongezeko la mimea hiyo vamizi katika hifadhi hiyo, limechangia kupungua kwa shughuli za utalii, kuzorotesha ubora wa ardhi na kupunguza ukubwa wa malisho.

Pia alisema kumechangia umaskini wa kaya hususani kwa wafugaji, kumeongeza migogoro baina ya wanyamapori na jamii na kuchangia kuongezeka kwa gharama za uhifadhi.

"Kwa hiyo matarajio ya mradi huu ambao nimegundua ni kupunguza mimea vamizi kwa asilimia 60 hadi 80, utapunguza matumizi ya kuni majumbani na utaongeza ajira," alisema Dk. Kimaro.

"Na utafiti huu ulipelekwa maabara na ikathibitika kwamba umekidhi viwango baada ya kuthibitishwa na TBS, kwa hiyo TAWIRI inatekeleza mradi huu kwa kushirikiana na Wana-Ikolojia wa Hifadhi ya Ngorongoro, na katika hatua za awali mradi huu umetengeneza kuni mbadala kutokana na mmea unaoitwa Makutian."

Pia alisema mradi huo ulishindanishwa katika mashindano ya Makisatu na kushika nafasi ya kwanza katika kundi la taasisi za utafiti Tanzania.

## Mwanafunzi agundua mfumo vipimo saratani

MWANAFUNZI wa mwaka wa nne kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Warda Islam, amegundua mfumo maalum ambao unasoma picha za vipimo kwa ugonjwa wa saratani na kutoa majibu papo kwa papo.

Akizungumza kwenye banda la DIT, mwanafunzi huyo alisema mfumo huo maalum unafanya kazi ya kusoma papo kwa papo majibu ya vipimo vya mgonjwa wa saratani tofauti na ule wa sasa ambao husubiri vipimo hivyo kusomwa na wataalamu na kutoa majibu kwa mgonjwa.

"Mfumo wa upimaji wa saratani unaotumika kwa sasa ni ule ambao mgonjwa huchukuliwa vipimo halafu vinapelekwa kwa wataalamu wa kusoma vipimo hivyo ambavyo hufanywa kwa mtindo wa picha na kisha kutoa majibu," alisema Islam.

"Lakini utofauti wa mfumo huu ambao nimegundua, wenyewe unatoa majibu papo kwa papo, yaani wenyewe mgonjwa anapokuwa anachukuliwa picha za vipimo, unakuwa unatoa majibu hapo hapo kama una saratani au laa na kama ipo imesambaa kwa kiwango gani."

Alisema mfumo huo aliogundua bado haujaanza kutumika na endapo utaanza kufanyakazi utasaidia kwa kiwango kikubwa kuokoa maisha ya watu wengi.

"Huu mfumo ukianza kutumika utaokoa maisha ya watu kwa sababu wenyewe hauhitaji upimwe halafu usubiri majibu kwa muda mrefu," alisema Islam.

"Nasema huu utaokoa maisha ya watu kwa sababu haupo kama unaotumika sasa ambao wakati mwingine unaweza kutumia muda mwingi kupatikana majibu ya vipimo kwa sababu wenyewe baada ya vipimo husubiri mpaka visomwe na mtaalamu, halafu yeye ndiyo atoe majibu ya kile alichokiona kwenye picha za vipimo husika, na kama ametingwa na shughuli nyingine inabidi avisubirishe jambo ambalo ni hatari kwa sababu endapo mtu ana saratani, kwa kipindi hicho anachosubiri inazidi kusambaa."

Warda alisema tayari mfumo huo umepelekwa Hospitali ya Ocean Road na kwamba majibu ya awali ambayo amepewa ni kwamba uko vizuri licha ya kumtaka afanyie maboresho madogo.

"Mfumo huu nimesha upeleka Ocean Road na wamethibitisha kwamba uko vizuri japokuwa wanataka ufanyiwe maboresho madogo ambayo tayari yamefanyiwa kazi, kwa hiyo walisema muda si mrefu watatupatia majibu ya hayo maboresho waliyosema tufanye," alisema Islam.

## Wananchi waondolewa hofu muda Vitambulisho vya Taifa

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imewatoa wasiwasi wananchi kwa hofu waliyokuwa nayo kuhusu kuisha kwa muda wa matumizi kwa vitambulisho vyake ilivyovitoa mwaka 2012.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye banda la NIDA, Msemaji wa Mamlaka hiyo, Geofrey Tengeneza, alisema hivi karibuni kumekuwa na hofu kwa wananchi kwamba huenda wakakosa huduma inayopatikana kutokana na vitambulisho hivyo walivyopatiwa awali wakati vinaanza kutolewa kuisha muda wake wa matumizi mwakani.

Alisema ni vyema wananchi wakatambua kwamba hakuna huduma watakazokosa baada ya vitambulisho vyao hivyo kuisha muda wa matumizi, kwa kuwa kinachozingatiwa ni namba pamoja na taarifa zilizotolewa awali na mmiliki husika wa kitambulisho.

"Nawaomba wasiogope kwamba vitambulisho vyao vinakwenda kuisha muda wake wa matumizi na watakosa huduma ambayo inapatikana kutokana na vitambulisho hivyo. Hata kama vitaisha muda wa matumizi huduma wataendelea kupata kama kawaida kwa sababu kinachoangaliwa sio gamba bali ni namba pamoja na taarifa za mtu husika," alisema Tengeneza.

Tengeneza alisema wapo pia ambao wamekuwa wakihoji sababu za NIDA kuweka muda wa kuisha matumizi kwa vitambulisho hivyo.

"Ni vyema wananchi wakatambua kuwa hili suala la kuwekewa muda wa kuisha matumizi ni la kawaida, kwa sababu tunaamini kwamba ndani ya miaka 10 huenda mmiliki wa kitambulisho kuna vitu vimebadilika kwake, aidha kama alikuwa hajaolewa, sasa ameolewa, kwa hiyo atahitaji kubadili taarifa zake," alisema Tengeneza.

"Kwa hiyo anapotaka kuhuisha kitambulisho chake ni lazima atataka kubadili na taarifa zake," alisema.

ama

ALHAMISI JULAI 7, 2022

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

Utajiri wa jotoardhi ulivyokamata rasilimali mazingira, nishati nchini



Ukurasa 13

Dk. Mzige: Hizi hapa haki 12 mgonjwa anazopaswa kuzijua



Ukurasa 14

Kanda Ziwa wanavyojipanga vita vikubwa kusambaratisha TB Sugu

AFYA

# Mjue alivyo aliye mzee zaidi duniani, utafiti nao ukiendelea watu wasizeeke

**Na Mwandishi Wetu**

Ni wastani zaidi ya miezi miwili imepita, mtu aliyesadikiwa kuwa na umri mkubwa zaidi duniani, Kiko Tanaka, amefariki umri wake ukilekea karne moja na robo.

Inarejea Ijumaa Januari 2, mwaka 1903 mtoto mchanga wa kike, alipozaliwa katika kijiji kidogo kisiwani, Kusini mwa Japan, sasa ameaga dunia akiwa na miaka 119. Hapo ndio jambo linaloibua swali, inawezekanaje kuishi miaka zaidi ya 100, akivuka wastani ulioko?

Kiko amefariki Aprili na miaka ya mwisho akirekodiwa na umri mkubwa zaidi duniani. Bibi huyo miaka ya mwisho amekaa katika nyumba ya wazee, ratiba ya maisha kila siku anaamka saa 12.00 asubuhi akifanya hesabu, michezo ya ndani, kula chokoleti, pia anakunywa kahawa na soda.



Ndivyo alivyokuwa marehemu Bibi Kiko Tanaka. **PICHA: MTANDAO**

Ratiba ya umri wa wazee wengi Japan, huanza ajira ya pili baada ya kustaafu ilivyozoeleka, Profesa Kiko ambayo ametumikia, akiwa mtaalamu mbobevu wa Sayansi ya Uzee au 'Gerontology'.

Bibi huyo profesa, ameshashika wadhifa, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Kisayansi la Japan katika Chuo Kikuu cha Tokyo, ikiwa kati ya nchi zinazoongoza kuwa na jamii inayozeeka.

Wastani wa umri wa kuishi Wajapani, sasa unatajwa kufika miaka 88 na wengi wa wananchi hao sasa wana umri zaidi ya miaka 65.

Inatajwa wengine wenye matarajio yanayofanana nao, ni mataifa ya Hong Kong, Singapore, Uswisi, Italia na Hispania.

Takwimu za Wizara ya Afya ya Japan, zinaonyesha idadi wenye miaka 100 au zaidi Japan, hadi mwaka jana walikuwa 86,510, ikiwa ongezeko zaidi ya watu 6,000, ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Kiko anataja kuishi miaka mingi kwao,ni zao la mengi, ikijumuisha, mfumo bima ya afya kufikia wote, huko kukitajwa kuna mfumo rahisi wa kupatikana huduma za afya tangu zama miaka 1960, wakisifiwa kuwa na mtindo sahihi kiafya.

Inatajwa, wengi huenda hospitalini kuchunguzwa afya kila mara, pia wanazingatia michezo katika maisha ya kila siku, taifa na wakazi wengi Japan sio wanene.

Hapo kuna ufafanuzi, bibi huyo msomi anasema ni zao la kupata mlo wenye mafuta kidogo, samaki, mboga, mizizi ya majini na chai kijani kibichi, raia wengi wakiegemea vyakula vya kawaida.

Bibi huyo anafafanua kwamba, umri wa wanaofanya kazi umeongezeka, idadi ya wenye umri miaka 65 na zaidi ni wengi, hasa kuzidi miaka 75.

Ni mustakabali wenye hoja, wazee pia wana mahitaji tofauti katika kukabidhinana madaraka nchini Japan, wakipatiwa haki hiyo inayowasaidia.

Bibi huyo alianza ajira ya pili akiwa na umri miaka 78, baada ya kutumikia chuo kikuu kwa muda mrefu. Anafafanua: "Nilipokuwa na umri miaka 70, nilianza ukulima. Kuna watu wanene nikiwemo mimi wenye ujuzi tofauti.

"Tulianzisha kampuni ambayo ilikopesha pesa nyingi na ardhi ya kilimo na tukaanza ukulima mdogo. Nilipokuwa mdogo nilitaka kuwa mkulima. Ilikuwa ni ndoto yangu ya miaka mingi."

Alipoulizwa hisia zake angependa kuishi miaka 100, akajibu: "Sina uhakika...mama yangu alifariki miaka mitatu iliyopita akiwa na umri wa miaka 98. Alikuwa na maisha mazuri, sina uhakika kama ninataka kuishi miaka mingi zaidi yake...Sina utashi sana wa kuishi miaka zaidi ya 100."

## WAZEE KUONGEZEKA

Muda wa kuishi Wajapani unatajwa umeongezeka na Mhadhiri Mwandamizi katika kituo cha Afya ya Wazee cha Aston, cha Birmingham nchini Uingereza, Cathy Slack, anasema ametafiti watu wanavyozeeka, kwamba unaweza kucheleweshwa kibaiolojia

Anafafanua dalili za nje za mtu kuzeeka, inajumuisha kusinyaa mwili, mvi na mengine chini ya ngozi yanayoleta tofauti, akiutaja kuwa mchakato binafsi na hakuna watu wanaozeeka sawa.

"Kuzeeka kusema kweli kunaathiri nyama katika mwili. Watu wengi hupata uzoefu wa kile kinachoitwa kupungua uwezo wa mwili kunakotokana na uzee katika maeneo mengi ya mwili wao kuanzia ubongo," anasema.

Anaitaja kuwa jambo lililopitwa na wakati kujaribu kuendeleza kuishi kwa afya ya awali na kukinga uzee akifafanua:"Sio kufanya kidogo au sana!.

"Dhibiti kiasi cha pombe unayokunywa, usivute sigara, huo ndio ushauri unaochosha ambao maofisa wa umma wamekuwa wakijaribu kutupatia kwa muda mrefu."

Anataja ni namna ya kuzisaidia chembehai zijikarabati upya, pia kupata usingizi kamili, huku wanasayansi wakiendelea kujifunza faida za vidhibiti uzee.

## KUCHELEWESHA UZEE?

Kitengo cha Idadi ya Watu cha Umoja wa Mataifa, kinakadiria kuwapo watu 573,000 katika mwaka 2021, shirika hilo linabashiri kuwa idadi hiyo itaongezeka.

Dk. Nir Barzilai, Mkurugenzi wa Taasisi ya Uzee, katika Chuo cha Tiba cha Albert Einstein, jijini New York Marekani, anafafanua ni kazi ngumu akiweka na kauli: "Katika maabara yangu, tunashuhudia kila siku mchakato wa kuzeeka ambao unaweza kucheleweshwa na mara nyingine unaweza kusitishwa."

***• Kwa mujibu wa mtandao.***

MAZINGIRA

WAKATI SERIKALI SASA IMEAMUA...

# Utajiri wa jotoardhi ulivyokamata rasilimali mazingira, nishati nchini

• Kona zote nchini zimejaa vyanzo

**Na Romana Mallya**

KWA miongo mingi Tanzania imekabiliwa na upungufu wa kuzalisha umeme wa kutosha, kutokana na sababu mbalimbali.

Pia, ziko hatua serikali imezichukua ili kutanzua tatizo la mgao wa umeme, ambazo kuna maeneo yameathirika kimazingira na ili kuepuka kujirudia matatizo hayo, serikali imeamua kuwa na vyanzo vya uzalishaji umeme vya nishati jadidifu, vikiwamo jua, upepo na jotokali.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara kutoka Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Shakiru Kajugus, anasema mwaka 2013 serikali ilianzisha kusimamia na kuongoza maendeleo ya jotoardhi, ikiwa ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

### MAANA YAKE NINI?

Mtaalamu huyo anafafanua: "Ni nishati safi na endelevu. Ni rasilimali inayojulikana pia kuwa nishati jadidifu kutokana na mfumo wa kutumika tena unaorudisha maji ardhini, baada ya mvuke kugeuzwa kuwa maji na kupoozwa na kwa desturi ya joto linalotoka chini ya ardhi, kwa kawaida halina kikomo."

Pia, anasema nishati hiyo huanzia kwenye ardhi isiyo na kina kirefu hadi kwenye maji ya moto na miamba ya joto iliyoko kina cha kilometa chache ardhini, zaidi kwenye miamba iliyoyeyuka kwa joto kali. Mhandisi Kajugus anafafanua: "Vipo vyanzo mbalimbali ambavyo kwa miaka mingi vimekuwa tegemeo la uzalishaji nishati kwa ajili ya viwanda na matumizi mengine.

"Miongoni mwa vyanzo hivyo ni maji, gesi, mafuta ghafi, makaa ya mawe na upepo, kutokana na uongezeko la uhitaji, baadhi ya nchi duniani mfano Kenya, Ethiopia, Iceland na Marekani zimepiga hatua katika uvunaji na utumiaji wa nishati ya jotoardhi."

Lingine analolitaja ni kwamba, Tanzania ni nchi inayopitiwa na Bonde la Ufa, pakiashiria mengine kama hifadhi ya rasilimali kubwa ya nishati, inayoweza kutumika kuzalisha umeme na mengine ya moja kwa moja.

Anasema nishati ya jotoardhi, inatokana na joto asilia linalozalishwa katikati ya ganda na kiini/kitovu cha dunia na husafiri kwa njia ya mpitisho ama msafara na kuhifadhiwa ndani ya ganda la dunia.

### WAPI INAPATIKANA?

Mhandisi Kajugus anataja maeneo yenye viashiria vya jotoardhi nchini, ni katika Kanda ya Kaskazini Ziwa Manyara (Manyara), Kreta ya Ngorongoro (Arusha), Ziwa Natron (Arusha) na Maji Moto (Mara).

Kanda ya Mashariki, anataja ni Utete - Rufiji na Luhoi (Pwani), Kisaki (Morogoro), huku Kanda ya Kusini kuna Songwe (Songwe), Ngozi na Kiejo-Mbaka (Mbeya) na Majimoto (Rukwa).



Kisima kifupi kilichochorongwa eneo la Kiejo – Mbaka, mkoani Mbeya. Kimeonyesha mafanikio makubwa ya upatikanaji wa nishati ya jotoardhi, kukitegemewa megawati 60 za umeme. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

> **Matumizi ya moja kwa moja huhitaji nyuzi joto 25 hadi 200, kiwango cha joto kinachohitajika kinategemea aina ya matumizi, mfano kukausha mazao kunahitaji nyuzi joto 38 hadi 95.**

Kanda ya Magharibi anapataja ni Ibadakuli (Shinyanga), Mtagata (Kagera) na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Dodoma, Singida na Tanga.

### UTAJIRI MEGAWATI

Mhandisi Kajugus anasema, Tanzania ina zaidi ya megawati 5000 za nishati hiyo zinazosubiri kuendelezwa, pakiwepo miradi mitano ya kuzalisha umeme wa joto, inayotarajiwa kukamilika mwaka 2025 kuzalisha megawati 200, zitakazoingia kwenye gridi ya taifa.

Miradi hiyo na kiasi kitakachozalishwa kwenye mabano ni Ngozi (75), Songwe (5), Kiejo-Mbaka (60) na Luhio (5) ambayo kuna hatua ya uhakiki rasilimali kwa kuchoronga visima, huku mradi wa Ziwa Natron ukitarajiwa kuzalisha megawati 60.

Katika Mradi wa Kiejo-Mbaka, kinachoendelea ni uchorongaji visima vifupi, huku programu ya kuchoronga visima vya uhakiki kwa mradi wa ngozi ukiendelea, pamoja na miradi ya majaribio ya matumizi mengine ya jotoardhi, inayotekelezwa Songwe.

### MATUMIZI YA NISHATI

Mhandisi Kajugus anataja matumizi yamegawanyika katika sehemu kuu mbili; moja ni kuzalisha umeme ardhini, kukiwapo mfano wa kuanzisha umeme, hitaji lake ni nyuzi joto kati ya 100 hadi 300.

"Matumizi ya moja kwa moja huhitaji nyuzi joto 25 hadi 200, kiwango cha joto kinachohitajika kinategemea aina ya matumizi, mfano kukausha mazao kunahitaji nyuzi joto 38 hadi 95," anasema Kajugus.

Anafafanua, matumizi ya moja kwa moja yanaweza kuchemsha maji kwa ajili ya matumizi majumbani na viwandani, kuotesha mimea kwenye nyumba za vioo (greenhouses), kukausha mazao, kupashia joto maji kwenye mabwawa ya samaki na kuua bakteria kwenye maziwa.

"Nishati hii inatumika kukausha mazao na kupasha moto nyumba ili kuongeza thamani ya mazao kama vile maharage, mchele, mbogamboga, matunda, mahindi, chai, kahawa, kokoa na mbao kulingana na uhitaji katika eneo husika," anafafanua.

### MANUFAA YALIVYO

Mhandisi Kajugus, anataja faida za ukaushaji mazao kwa nishati ya jotoardhi, inapunguza mazao yanayopotea shambani na nyumbani wakati wa ukaushaji.

Lingine, ni kuongezeka ubora wa kinachozalishwa, kuondoa matumizi ya dawa ghalani na kuongeza thamani ya mazao sokoni, huku kukipasha joto nyumba kitalu, faida yake inagusa kuongeza uzalishaji, kupunguza matumizi ya dawa kitaluni, kuzuia uzalishaji fangasi kwenye mazao na kuongeza tija na thamani kwa mkulima.

Katika ufugaji samaki, anasema nishati hiyo inatengeneza mazingira sahihi na salama kwao kukua, hata kukidhi kiwango kinachohitajika sokoni, hivyo kuongeza tija na thamani kwa mfugaji.

### MAHITAJI MAHSUSI

Mhandisi huyo anasema, nishati hiyo ina madini inayoambatana na inatumika kutibu magonjwa ya ngozi kama harara, miwasho, upele, mapunye na fangasi miguuni.

Anasema viwandani inatumika kupasha mitambo, kukausha samaki, kuosha chupa za maji viwandani na kuhudumia gesi (CO2) inayohifadhi vinywaji kama soda, na bia.

Vilevile, anasema nishati hiyo inaongeza thamani katika utengenezaji vyakula, kulainisha maganda ya matunda na mboga na kuzimenya, huku ikizalisha chumvi za majumbani, inatajwa kutumika moja kwa moja kwa mengi.

### NINI KINAFANYIKA?

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, anasema Tanzania ina maeneo 52 yaliyokwishatanuliwa na yanafaa kutoa nishati ya jotoardhi.

Anasema nchi itazalisha umeme kiasi cha megawati 200 zinazotokana na jotoardhi hadi kufika mwaka 2025, akifafanua: "Serikali ina mpango wa kuongeza megawati 1100 zinazotokana na nishati jadidifu kabla ya mwaka 2025 na hizo megawati zitatokana na vyanzo mbalimbali kama vile jotoardhi, jua na upepo.

"Wizara ya Nishati inaweka nguvu kubwa katika kuendeleza vyanzo vya nishati ya jotoardhi kwa sababu vyanzo hivyo haviishi, kipindi cha ukame maji yanaweza kupungua, lakini jotoardhi, mvuke unaotoka chini ya ardhi uko palepale," anaeleza Kajugus.

Anatoa mfano linganishi, Kenya ina zaidi ya megawati 1,100 zinazotokana na jotoardhi, huku Tanzania kutokana na eneo kubwa kupitiwa na Bonde la Ufa, kuna uwezekano kupata umeme mwingi unaotokana na nishati hiyo.

Anasema mkoa wa Mbeya eneo la Rungwe kumebainika uwezekano mkubwa wa kutoa nishati jotoardhi, kwa sababu tawi moja la Bonde la Ufa limeingia mahali hapo na lingine limeelekea nchi jirani, Malawi.

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba, anasema eneo la Kiejo-Mbaka linaweza kuzalisha megawati 60 zinazotokana na jotoardhi na kwamba serikali imetoa takribani Sh. bilioni 20 kwa ajili ya uendelezaji wa eneo hilo.

Anasema katika eneo la ngozi, inategemewa kuzalisha megawati 70 zinazotokana na Jotoardhi.

AFYA

# Dk. Mzige: Hizi hapa haki 12 alizonazo mgonjwa na anapaswa kuzijua vema

**Na Flora Wingia**

JAMBO moja muhimu ambalo watu wengi hawalijui au hawalitilii maanani, ni kwamba wagonjwa wana haki zao. Hiyo ni kwa mujibu wa Dk. Ali Mzige, Daktari Bingwa wa Afya ya Jamii na Familia nchini.

Anasema nchi nyingi duniani, akitaja mifano ya Uturuki, Denmark, Hungary, Malaysia, Japan, Marekani, Afrika Kusini na Uingereza, wanayo maandiko ya kitaifa yanayoainisha haki za wagonjwa.

Maandiko kama hayo, yanaeleza haki za kila mtu mgonjwa anayehitaji huduma za tiba, ili kulinda hadhi, utu na heshima na Shirika la Afya Duniani (WHO), linafahamu na kubaini kuwa unyanyasaji na unyanyapaa unaweza kujitokeza katika masuala ya tiba.

Kwa mantiki hiyo, liliandaa siku za awali kwenye miaka ya 1948, haki za wagonjwa zenye vipengele 12. Ikianza na mgonjwa kupewa haki ya kupewa tiba yenye heshima.

Pili, mgonjwa anayo haki ya kupata taarifa kamili na iliyo sahihi kutoka kwa tabibu kuhusu ugonjwa wake katika njia atakayoweza kuelewa. Endapo taarifa hiyo ni tete na itamletea mgonjwa usumbufu, taarifa hiyo apewe mtu aliye karibu na anayemhusu kwa niaba yake.

Dk. Mzige anataja mgonjwa anayo haki ya kumfahamu kwa jina daktari wake ambaye anamtibu na ambaye pia ndiye anayeratibu matibabu yake.

Nne, mgonjwa huyo anataja haki ya kupewa taarifa kutoka kwa tabibu au daktari wake, zitakazomwezesha kutoa idhini au rai kuhusu uchunguzi na tiba yoyote kabla ya kufanyika.

Hapo inatajwa, endapo ipo haja ya kujadili au kutoa tiba tofauti na ile ya awali kama ipo, mgonjwa atabakiwa na haki ya kupewa taarifa hiyo, vilevile, mgonjwa anakuwa na haki ya kumjua kwa jina atakayefanya tiba au uchunguzi huo unaotarajiwa kufanyika.

Dk. Mzige anakumbusha, mgonjwa ana haki ya kukataa tiba kwa mujibu wa kanuni na sheria zilizopo na pia anapaswa kuelezwa nini hatma yake kitiba, kwa hatua aliyoichukua.

Tano, anataja mgonjwa ana haki ya kufikiriwa kuhusu usiri wa tiba na huduma zake kwa ujumla katika maendeleo ya matibabu yake, kuzungumzia hadharani kwa njia ya ushauri, pia kumpima ni siri ya mgonjwa na wasiohusika, hususan wanafunzi au jopo la madaktari, wanapaswa kupata ridhaa ya mgonjwa au mlezi wake.

Haki ya sita tabibu huyo anaitaja, ni mgonjwa anatakiwa kuwa na mawasiliano yake na kumbukumbu zake zote zinazohusu ugonjwa na tiba zinahifadhiwa kama nyaraka za siri.

Saba, inatajwa mgonjwa anastahili haki ya kutarajia kutokana na uwezo wake, hospitali lazima ifanye jitihada za kuweza kumhudumia mara anapohitaji tiba au huduma.

Katika hilo, hospitali inatajwa ni lazima ifanye tathmini kuhusu huduma na kama ilivyo wakati wa dharura, ikibidi rufani iwe ni kitu cha haraka au pale inapobidi kama mgonjwa atapewa rufaa ya kwenda hospitali nyingine.

Hayo yapaswa yafanyike baada ya mgonjwa kupewa taarifa kamili kuhusu sababu za rufaa iliyopendekezwa na endapo kuna huduma nyingine badala ya hiyo rufaa. Taasisi au asasi itakayopokea uhamisho wa mgonjwa, lazima ikubali kwanza kumpokea.

Nane, inatajwa mgonjwa kuwa na haki ya kupata uhusiano uliopo kati ya hospitali inayomtibu na huduma nyingine zilizopo kama vyuo vya taaluma. Pia, anayo haki ya kujua uhusiano uliopo kitaaluma kati ya wataalamu wanaomtibu kwa majina.

Tisa, kuna haki ya mgonjwa kuwa na haki ya kupewa ushauri kama hospitali ina mpango wa kufanya utafiti wowote au majaribio yoyote yanayohusu binadamu, ambayo huenda yakaathiri tiba na huduma anazopewa hapo hospitalini. Mgonjwa anayo haki ya kukataa kushiriki katika tafiti hizo.

Fursa ya 10 inayotajwa, ni kwa mgonjwa kuwa na haki ya kutarajia kuwa tiba yake itakuwa endelevu isiyo na kikomo na mgonjwa ana haki ya kujua muda anaopewa ahadi ya kumuona daktari au mtoa huduma na itamlazimu mtoa huduma awepo kwa wakati uliopangwa.

Mgonjwa katika haki alizo nazo, ni lazima apangiwe atakayechukua nafasi ya tabibu mhusika, endapo tabibu hatakuwepo. Haki za mgonjwa hazikomi njiani, bali wakati akipewa ruhusa kwenda nyumbani, apewe nyaraka zote za kutoka hospitali.

Gwiji huyo wa tiba nchini, anasema haki ya 11, inaangukia mgonjwa anayetibiwa katika hospitali binafsi, anayo haki ya kujua na kuelezwa mchanganuo wa gharama anazopaswa kuzilipa na siyo lazima ijulikane fedha hizo zinatoka wapi.

Inawezekana kuna mtu atakayemlipia. hata kama unadhani huenda hana uwezo wa kumlipia bili.

Haki ya 12. Dk Mzige anaitaja kwamba ni mgonjwa anastahili kujua kanuni, sheria na utaratibu uliopo katika hospitali anayotibiwa, ili azifahamu.

Kwa wauguzi wote na wahudumu wote wanaotoa tiba na huduma kwa wagonjwa, Dk. Mzige anasema majukumu yao makubwa ni mawili, kama watoa huduma, pia wao ni wagonjwa watarajiwa. Hapo anasisitiza kwamba, wanapaswa kujua sheria, pia kanuni kuhusu hizo za haki ya mgonjwa.

**HAKI IKOJE NCHINI?**

Katika swali hilo la Nipashe kwa Dk. Mzige kutaka kujua kama haki hizi zipo nchini, anajibu kwamba 'sina jibu la haraka'.

Katika nchi zilizoendelea, mara nyingi haki za mgonjwa zimepewa kipaumbele kwa sababu ya elimu inayoufikia umma, ikianza na kujua haki za kila mmoja. Hapo Dk. Mzige anafafanua: "Siyo wote wanaojua haki za mgonjwa. Rushwa inapojitokeza katika huduma za jamii, haki za mgonjwa zinatiwa mfukoni."


Profesa Kisali Pallangyo, aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo cha Muhimbili cha Sayansi na Tiba, mnamo Julai 5, 2012, alitoa taarifa kwa vyombo vya habari wakati wa migomo ya madaktari kama alivyonukuliwa gazetini kwa kauli:

"Iko haja kwa sisi tukiwa madaktari na matabibu, kufuata maadili yetu ya kidaktari kwa kuwajali na kuwahudumia wagonjwa na kuhakikisha kuwa tunawaondolea maumivu wanayoyapata, wakiwa pia wanategemea tutaboresha siha zao na kuokoa maisha yao".

Maandiko hayo, kwa mujibu wa Dk. Mzige, ni mazito na yanataka jamii itafakari tunakwenda wapi katika elimu yetu ambayo dunia inajua kuwa uhai wa binadamu unaboreshwa na utoaji wa elimu kwanza, akisisitiza umma wote ni wagonjwa, ikijumuisha madaktari na wauguzi.



Daktari akimhudumia mgonjwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Dk. Ali Mzige.

> **Iko haja kwa sisi tukiwa madaktari na matabibu, kufuata maadili yetu ya kidaktari kwa kuwajali na kuwahudumia wagonjwa na kuhakikisha kuwa tunawaondolea maumivu wanayoyapata.**

AFYA

# Kanda Ziwa wanavyojipanga vita vikubwa kusambaratisha TB Sugu

• Bosi Kibong'oto ataja shida, mbinu kukabili

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UGONJWA wa Kifua Kikuu (TB) huandamana kwa karibu sana na ugonjwa wa Ukimwi na malaria. Ni kati ya magonjwa yanayochangia vifo vingi nchini na wengi wamekuwa wakiugua bila ya kujua, wanakimbilia kwa waganga wa jadi wakidhani wamerogwa.

Dalili za kifua kikuu kwa watoto zinaonekana kuwa sawa na magonjwa mengine na watoto hawawezi kueleza matatizo yao, hivyo mara nyingi huchelewa kuutambua ugonjwa, au hata wazazi wakipuuza.

Mapambano dhidi ya kifua kikuu yameendelea kuchukua nafasi muhimu nchini na miongoni mwa makundi yanayoathirika ni watoto wa umri hadi miaka14, kundi lililo hatari kueneza maradhi hayo zaidi.

Hadi sasa, Tanzania inatajwa kuwapo katika kundi lenye wagonjwa wengi wa kifua kikuu. Hiyo inafanya serikali kuja na mikakati ya kupunguza idadi ya wagonjwa hao, ni pamoja na kusambaza mashine za kupima na kutoa majibu ndani ya masaa mawili.

Mkakati wa Shirika la Misada la Marekani(USAID) inayoendele dhidi ya kifua kikuu nchini, unasaidia Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) kushughulikia changamoto za kimfumo na kiutendaji kuzuia, kugundua na kutibu ugonjwa huu hatari.

Pia, hiyo inatajwa ni pamoja na kuboresha upatikanaji huduma bora, inayozingatia wagonjwa wa kifua kikuu sugu kuzuia maambukizi na mwenendo wa ugonjwa na kuimarisha majukwaa ya kifua kikuu, ili kupunguza utegemezi wa ufadhili kwa fedha na utaalamu.

Katika kuendelea kupamba na TB, serikali kupitia Wizara ya Afya imekutana na Waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma ngazi ya Mikoa na Wilaya za Kanda ya Ziwa, kukumbushana wajibu wa kukabiliana na changamoto hiyo, kikao kilichofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

### MKURUGENZI KIBONG'OTO

Dk. Leonard Subi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali Maalum Ngazi ya Taifa ya Tiba ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, anasema asilimia 70 ya wagonjwa wa TB wanaripoti katika vituo vya afya na kupata matibabu, huku asilimia 30 wakiwa bado mitaani na baadhi yao wanakimbilia kwa waganga wa jadi.

Anasema wagonjwa wa TB wengi wanashinda kwa waganga wa jadi na kuambukiza wengine wanaofika sehemu hizo na waganga hao wa jadi, hawana vipimo vya kumtambua mgonjwa



Kampeni dhidi ya kifua kikuu ikiendelea wilayani Kahama. **PICHA: MTANDAO**

> **Lazima mgonjwa wa TB wakati wa matibabu yake tushirikiane na wanafamilia yake, kuhakikisha anapata matibabu ipasavyo. Zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa wa TB sugu wanapona hivyo dawa zetu zinafanyakazi vema.**

huyo.

Dk. Subi anasema, wastani wa theluthi moja ya wagonjwa bado hawapati tiba hospitalini na anawasihi waratibu hao kuwa waibuaji wazuri wa wagonjwa katika maeneo yao wanapotaka kuwapatia elimu wananchi, ili wafahamu TB ni nini, dalili zake na kuwajuza serikali inagharimia matibabu yote bure.

Aidha, anasema serikali imeshatoa mashine za kugundua mgonjwa wa kifua kikuu haraka ndani ya saa mbili, kwani kipindi cha nyuma walikuwa wakigundua ugonjwa kwa huo kwa muda wa siku mbili hadi tatu, hali iliyosababisha mgonjwa kuchelewa matibabu.

Dk. Subi anasema, kila Mratibu wa ugonjwa huo anatakiwa kuwaibua wagonjwa na kuwapatia tiba, ili wasiendelee kukimbilia waganga wa jadi. Hali inayoweza kusaidia kukata mnyororo wa uambukizaji wa ugonjwa huo.

Anasema kuibua wagonjwa hao kunatakiwa kwenda sambamba na utoaji elimu ya ugonjwa huo na dalili zake, kuwafuatilia baada ya kuanza matibabu na kwa mgonjwa atakayehudhuria vipindi vyote vya matibabu, serikali itampatia Sh.100, 000 sehemu ya usafiri na lishe.

"Lazima mgonjwa wa TB wakati wa matibabu yake tushirikiane na wanafamilia yake, kuhakikisha anapata matibabu ipasavyo. Zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa wa TB sugu wanapona hivyo dawa zetu zinafanyakazi vema," anasema Dk. Subi.

### KUTOKA WIZARANI

Yusto Erasto, ni Ofisa Mtakwimu kutoka Wizara ya Afya anasema, wagonjwa wa TB ni



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali Maalum Ngazi ya Taifa ya Tiba ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto Dk. Leonard Subi, akizungumza na Waratibu wa Kifua Kikuu (hawapo pichani) Kanda ya Ziwa, mjini Kahama. **PICHA: SHABAN NJIA**

wengi, lakini wanaofika katika vituo vya afya kupata matibabu ni wachache, hivyo ni lazima kuwa na mikakati kuhakikisha wanafikiwa na kupata matibabu.

Anasema, kila mratibu wa ugonjwa huo anatakiwa kutumia mfumo wakati wa kuhamisha mgonjwa wake wa TB na sio kutumia mfumo wa maandiko pekee, kama ilivyokuwa awali bali amfuatilie kujua hali yake ya matibabu, kudhibiti hali.

"Wagonjwa wengi wamekuwa wakihama vituo vyao, lakini hakuna ufuatiliaji ili kujua kama bado anaendelea kutumia dawa zake ipasavyo au la. Hii imekuwa ikisababisha kuwa na wagonjwa wenye TB sugu," anasema Erasto.

Mratibu wa TB na Ukoma kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Mageda Pastory, anasema wagonjwa wa maambukizi ya virusi vya Ukimwi, huchangia kupatikana TB, hivyo ni lazima kuwafuata katika maeneo yao wapate elimu stahiki ya TB na dalili zake, kisha wanatibiwa.

### WARATIBU WA TB

Daniel Mihayo, ni Mratibu wa TB Kanda ya Ziwa, anasema serikali imekuwa ikifanya kazi na waganga wa jadi kwa kuwapatia elimu ya utambuzi wa dalili za ugonjwa huo, ili wanapopata wateja wenye dalili mojawapo wawaripoti katika vituo vya afya kwa matibabu zaidi.

Anasema, katika ofisi za waganga hao sasa, pia wamebandika mabango yanayoonyesha mtu mwenye dalili za kifua kikuu anakuwaje, hapo wanashirikiana na watoa huduma ngazi za jamii kufikisha elimu kwa wananchi na kuchukua sampuli za makohozi, kwenda kupima na kurejesha majibu.

Mihayo anasema, wameanzisha huduma ya kliniki tembezi inayozunguka sehemu mbalimbali kutoa elimu na kupima wagonjwa wa TB na wanaobainika wanalazimika kuwapiga picha za 'X-ray' kujiridhisha kuhusu kuumwa kwao.

Dk. Magdalena Kweka, kutoka Hospitali ya Rufani Bugando, Mwanza, anasema wamekuwa wakitoa elimu ya ugonjwa wa TB siku ya maadhimisho ya ugonjwa huo na kuwapima, wakiwamo kundi la wenye virusi vya

HIV pale wanapohudhuria ratiba za kliniki zao.

Mratibu, Mariamu Mabaga, kutoka Manispaa ya Kahama, anasema wamefanikiwa kuwapatia elimu ya utambuzi wa wagonjwa wa TB na dalili zake, waganga wa jadi watano na wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ikiwa ni sehemu ya mapambano yao

Mabaga anasimulia, wanatoa mafunzo hayo baada ya kuwepo mila potofu kwa wagonjwa wa kifua kikuu kukimbilia waganga wa jadi kutibiwa kienyeji, kwa madai kuwa wamerogwa jambo lilipokuwa hatari kwa afya zao na watu wanaowazunguka.

Anasimulia, kati ya waganga wa jadi watano waliopatiwa mafunzo ya dalili za ugonjwa wa kifua kikuu, wawili pekee ndio wamekuwa wakitoa ushirikiano kwa watoa huduma wa afya kwa kutoa taarifa za wagonjwa wanaofika katika maeneo yao kupatiwa matibabu.





## Mavunde atoa somo kuhusu upandaji miti

Na Renatha Msungu, DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, ameitaka jamii kujenga utaratibu wa kupanda miti badala ya kusubiri matukio ya kitaifa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza jana kwenye upandaji miti ulioandaliwa na Taasisi ya Habari Development kwa udhamini wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kwenye eneo la Mirembe jijini hapo, Mavunde alisema upandaji miti unapaswa kuanzia ngazi ya familia.

"Naomba jamii ijifunzeni na kuweka utaratibu wa kupanda miti, iwe ya matunda na miti mingine ili kuboresha mazingira katika maeneo wanayoishi," alisema Mavunde.

Hata hivyo, Naibu Waziri Mavunde aliwapongeza wadau hao kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kukijanisha Dodoma.

"Zoezi hili la upandaji miti liwe endelevu na kuwataka wasiishie eneo hilo tu wajitokeze kwenda kupanda na maeneo mengine kwa sababu miti ni uhai na inasaidia kuleta kivuli kwa jamii," alisema.

Katika hatua nyingine, Mavunde aliwataka wakazi wa jijini Dodoma kuendelea kupanda miti katika maeneo mbalimbali ili kukabiliana na athari za mazingira.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema kampuni yake imefanya hivyo ili kuunga mkono jitihada za serikali za kuboresha mazingira ya Dodoma.

Alisema wataendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali kuhakikisha wanaunga mkono jitihada za serikali za upandaji miti na kuwataka wananchi waendelee kupanda miti.

Aliipongeza pia Habari Development kutokana na kuja na wazo la upandaji miti kwa ajili ya kuhakikisha wanaikijanisha makao makuu.

**"Naomba jamii ijifunzeni na kuweka utaratibu wa kupanda miti, iwe ya matunda na miti mingine ili kuboresha mazingira katika maeneo wanayoishi," alisema Mavunde.**

# Fedha za UVIKO- 19 zamaliza kero maji

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAKAZI wa Ntyuka-Chimalaa jijini Dodoma wameondokana na kero ya maji ya muda mrefu baada ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Dodoma (DUWASA), kukamilisha ujenzi wa mradi uliotekelezwa kupitia fedha za maendeleo ya ustawi na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Mradi huo umegharimu takribani Sh. milioni 471.8 na fedha za UVIKO-19 zilikuwa Sh. milioni 359.7 na Sh. milioni 112 zimetolewa na mamlaka hiyo kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato.

Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, aliyasema hayo jana wakati Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma ilipotembelea kukagua mradi wa maji Ntyuka Chimalaa.

Alisema wananchi wa eneo hilo walikuwa hawana kabisa huduma ya maji safi, hivyo kulazimika kutembea umbali wa kilometa tano hadi saba kufuata huduma hiyo maeneo mengine.

"Serikali kwa kutambua athari za ugonjwa wa UVIKO-19, imetenga fedha za utekelezaji wa mradi wa mfumo wa majisafi eneo la Ntyuka Chimalaa. DUWASA ilipokea Sh. milioni 359.7 lakini hazikutosha kukamilisha mradi mpaka kufikisha maji kwa wananchi, hivyo kupitia makusanyo ya ndani tuliongeza Sh. milioni 112," alisema. Mkurugenzi huyo alisema mradi umetekelezwa ndani ya miezi sita na utanufaisha wakazi 4,558 wa eneo hilo.

"Upatikanaji wa maji kwa sasa umetoka asilimia sifuri hadi 95. Tunashukuru serikali kwa kutoa fedha kutekeleza miradi ya maji na kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji maeneo mbalimbali Dodoma," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa Mkoa wa Dodoma, Damas Mukasa, alitoa rai kwa wananchi kujitokeza kuwasilisha maombi ya kuingiziwa maji kwenye nyumba zao na kuwataka kutunza mradi huo ili udumu na kutoa huduma endelevu.

"Tunashukuru Kanisa la Anglikana kwa kutoa eneo hili bure la huu mradi. Sasa wananchi wenzangu tujiepushe na uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji na hii miundombinu ni muhimu kuitunza ili mradi wetu udumu," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alishukuru serikali kwa kuwatua ndoo kichwani kinamama waliokuwa wakipata adha kubwa ya maji kwa kutembea umbali mrefu na wakati mwingine kununua ndoo kwa Sh. 100 kwa wanaowapitishia kwenye mikokoteni.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Dk. Damas Mkassa (kulia), akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa wakazi wa mtaa wa Chimalaa Kata ya Ntyuka jijini humo baada ya Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa kutembelea juzi kwa ajili ya kukagua mradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA). **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bashe azindua kituo huduma kwa wakulima

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amezindua kituo cha huduma kwa wateja wakulima kwa ajili ya kupiga simu ili kupata taarifa na utaalamu wa masuala ya kilimo.

Akizindua kituo hicho juzi, Bashe alisema wakulima watakuwa wakipiga simu bure ili kupata taarifa na kuuliza maswali yanayohusiana na kilimo na kuwafikia popote walipo nchini.

Alisema jambo hilo ni mwanzo wa kuelekea hatua kubwa ya mafanikio na wakulima watakuwa wakipata taarifa ya mazao gani yanatakiwa sokoni ili kulima kwa wingi.

Bashe alibainisha kuwa awali walikuwa wakisikiliza matatizo ya wakulima kwa njia ya ujumbe mfupi lakini sasa yatasikilizwa kwenye simu na kutunza taarifa zao.

Kwa mujibu wa Bashe, baada ya mfumo wa huduma kwa wateja kukamilika kama nchi lazima kuwe na kitengo kilichosajiliwa cha masoko ili kuangalia bei kwenye soko zinakwendaje.

"Ifike mahali wizara iwe na kitengo chenye nguvu cha kuingia kutafuta masoko ili kufanya mazao yetu yawe na ushindani kwenye soko," alisema.

Waziri Bashe alihimiza kituo hicho kufanya kazi kwa saa 24 na kiwe na mfumo unaotunza taarifa.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema kazi kubwa imefanyika ya kuiweka wizara kiganjani na kwamba mkakati uliopo ni kuanzishwa kwa 'channel' maalum kwa ajili ya kilimo.

Mavunde alisema kuwa kupitia kituo cha huduma kwa wateja, wakulima watapata taarifa za kilimo kila siku na wakulima wengi watafikiwa.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Andrew Massawe, alisema takwimu zinaonyesha mfumo wa M-Kilimo umesaidia kwa kiasi kikubwa wakulima.

Massawe alisema wakulima milioni 5.5 kupitia mfumo huo wamesajiliwa huku wauzaji wa nje waliosajiliwa ni 3,905 na kwamba tayari wametatua kero 60,120 za wakulima.





# Majeruhi saba ajali ya lori wapokelewa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), imepokea majeruhi saba wa ajali ya gari iliyohusisha lori lilokuwa limebeba shehena ya mahindi likitokea mkoani Songwe kuelekea jijini Dar es Salaam ambalo lilishindwa kufunga breki eneo la Inyala na kuparamia gari dogo la abiria aina ya Coaster lililokuwa likitokea jijini Mbeya kuelekea Ubaruku, Wilaya ya Mbarali.

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 10 jioni na watu watano walipoteza maisha papo hapo huku wengine wakikimbizwa hospitali.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Godllove Mbwanji, wamepokea majeruhi saba kati yao watano ni wanawake na wawili ni wanaume, wote hali zao zinaendelea vizuri.

"Tunamshukuru Mungu hali za majeruhi zinaendelea kuimarika tuliwapokea wakiwa katika hali tofauti, lakini jitihada za madaktari wetu zimesaidia afya zao kuelekea vizuri, tunatoa pole pia kwa ndugu jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao katika ajali hiyo," alisema Dk. Mbwanji.

Katika taarifa yake juzi kwenye eneo la tukio, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, Ulrich Matei, alilitaja lori hilo kuwa ni lenye namba za Usajili T.317 DWL na tela namba T.804 BMF ambalo liligonga basi lenye namba za usajili T. 201 DUN.

Kamanda Matei alisema baada ya lori hilo kuligonga basi lililoburuza mpaka kwenye makazi ya watu, dereva wa lori hilo bado hajulikani alipo.

"Idadi ya majeruhi bado hatujaipata, lakini nikitoka hapa naelekea hospitali kwa ajili ya kufuatilia idadi yao na hali zao maana taarifa za awali ni kwamba wengi wao wameumia sana," alisema Matei.

Kamanda Matei alisema chanzo cha ajali hiyo ni wembamba wa barabara na wamewasiliana na Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), kupanua barabara hiyo.

Alisema wembamba wa barabara hiyo katika eneo la Inyala hadi Tazama Pipeline, unasababisha ajali za mara kwa mara kutokana magari kushindwa kupishana inapotokea dharura.

Mmoja wa mashuhuda, Joseph Mwanganya, alisema alishuhudia wakati lori hilo likianza kuligonga gari dogo mpaka lilipovamia vibanda na kwenda kuvamia nyumba moja iliyopo pembeni.

Alisema lori hilo baada ya kushindwa kufunga breki lilishindwa kulikwepa basi la abiria kutokana na barabara hiyo kuwa nyembamba.

Julieth Mvungi alisema yeye ni mwathirika katika ajali hiyo kwa kuwa nyumba yao iligongwa na lori na kuvunja vitu mbalimbali vilivyokuwamo ndani.



Baadhi ya maofisa wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya wakikusanya baadhi ya mabaki ya miili ya watu waliofariki kwenye ajali iliyohusisha lori la mizigo lililogonga basi dogo la abiria katika eneo la Inyala nje kidogo ya Jiji la Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mfumo mpya utoaji vibali kusafirisha mifugo wafurahiwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MFUMO mpya wa utoaji wa vibali kielektroniki kwa ajili ya kusafirisha mifugo na bidhaa zote zitokanazo na mifugo pamoja na uvuvi umeanza kutumika na kusifiwa na wafanyabishara mbalimbali kwamba unaokoa muda.

Mfumo huo ulitangazwa kutumika rasmi Julai mosi, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali nchini na unalenga kuongeza ufanisi na kuokoa muda kwa wafugaji na wafanyabiashara kuuza mifugo na bidhaa mbalimbali zinazotokana na mifugo.

Mfumo huo ulizinduliwa hivi katibuni jijini hapa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia mifugo, Tixon Nzunda, aliyesema mfumo huo wa kielektroniki unalenga kuondoa urasimu, vitendo vya rushwa na uzembe uliokuwa unafanywa na baadhi ya wataalam wanaoshughulikia upatikanaji wa vibali.

Alisema, utarahisisha shughuli za utoaji vibali kwa njia ya mtandao na wafanyabiashara hawatapanga tena foleni kwa wataalam wakiwamo maofisa ugani kushughulikia vibali vya kusafirisha mifugo na mazao yatokanayo na mifugo badala yake watatumia teknolojia za simu na kompyuta.

Alisema, serikali ilianzisha mfumo huo ukiwa na lengo la kuokoa na kukusanya mapato yatokanayo na ukataji wa vibali na kuwabana watumishi waliokuwa wakiendekeza rushwa na urasimu kuwahudumia wananchi.

"Tunajivunia kuona sasa tumefanikiwa kuanzisha mfumo wa kielekroniki ambao utatumika kutoa vibali vya usafirishaji wa mifugo na bidhaa zake, kama vile ngozi, mayai na nyama kutoka kila pembe ya nchi huko aliko apate kibali chake kupitia simu yake ya mkononi na kuendelea na shughuli zake," alisema Nzunda.

Pia, wameamua kuutambulisha mfumo huo kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hususani mkoani Mbeya kwa kuwa ni eneo ambalo linawafugaji wengi wanaofuga kisasa na kuzalisha maziwa yenye ubora unaokubalika kimataifa.

Kwa upande wake, Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Daniel Mushi, alisema mfumo huo utamewarahisishia wafanyabiashara wa nyama nchini kupata vibali kwa wakati na kufanya shughuli zao kwa uhuru.

Alisema mfumo huo utapunguza mlolongo mrefu wa kufuatilia vibali katika ofisi za serikali na badala yake vitakatwa kielektroniki. Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Trade Mark East Afrika, Lilian Masalu, alisema walishawishika kuisaidia serikali kuanzisha mfumo huo baada ya kuona ucheleweshwaji wa vibali vya kusafirisha mifugo hali iliyokuwa inasababisha bidhaa zitokanazo na mifugo kuharibika na wafanyabiashara kuingia hasara.

Alisema mfumo huo utakuwa na tija kwa mfugaji na mfanyabiashara ambao kwa pamoja watauza kwa wakati na kujiingizia kipato.

Baadhi ya wafanyabiashara, akiwamo Jackson Gwamaka, anayejishughulisha na uuzaji wa ngozi, walisema mfumo wa kuomba vibali kielekroniki umewasaidia kupanga bei ya pamoja nchini kuliko ilivyokuwa awali kila wilaya kupanga bei zake za kuomba vibali.

## Ukosefu chakula shuleni chanzo wanafunzi kufeli

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

UKOSEFU wa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi, wilayani Mbarali, umetajwa kuwa sababu ya watoto wengi kushindwa kumudu masomo yao na kuchangia kufanya vibaya kwenye mitihani.

Hali hiyo imewaibua wadau wa elimu na kuiomba Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kutunga sheria ndogo itakayowalazimisha wazazi kutoa chakula kwa ajili ya watoto wao kwa lazima.

Akizungumza kwenye kikao cha wadau wa elimu wilayani Mbarali juzi, Mratibu wa Elimu Kata ya Mapogoro, Francis Makombe, alisema mara kwa mara wanahamasisha wazazi pamoja na walezi kuchangia chakula shuleni, lakini wamekuwa wakaidi.

Alisema licha ya wilaya hiyo kuwa wazalishaji wakubwa wa zao la mpunga, mwitikio ni mdogo na kusababisha pia watoto kufanya vibaya kwenye mitihani yao kutokana na kukosa chakula shuleni.

Alisema kutungwa kwa sheria ndogo kutasaidia kuwabana wazazi na kulazimika kuchangia chakula kwa lazima na wakaidi watachukuliwa hatua.

"Tumejitahidi sana kuwahamasisha wazazi pamoja na walezi kuchangia chakula shuleni, tumetumia mikutano ya hadhara na mikusanyiko mingine ili kuhamasisha zoezi hili, lakini bado mwitikio ni mdogo, nafikiri tukitunga sheria ndogo za kuwabana itasaidia chakula kipatikane kuliko ilivyo sasa tunabembeleza wakati elimu ni kwa manufaa ya watoto wetu na jamii," alisema Makombe.

Diwani wa Mapogoro, Paul Kitta, alisema atapeleka hoja ya dharura kwenye vikao vya baraza la madiwani kutoa tamko juu ya wazazi kuchangia chakula shuleni pamoja na kutungwa kwa sheria ndogo.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kuwapo chakula shuleni ambao utasaidia watoto kusoma kwa utulivu kwa kuwa hawatakuwa na njaa na kuelewa masomo ya mchana.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Misana Kwangura, alisema kupatikana kwa chakula shuleni kutakuwa ni mwarobaini wa kuongeza ufaulu kwa watoto na kuifanya wilayani hiyo kushika nafasi za juu kitaaluma.





# EAC yapewa jukumu katika kukuza lugha ya Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Sanaa na Utamaduni ameiomba Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) kuongeza juhudi zaidi kuhakikisha lugha ya Kiswahili inatumika kikamilifu katika nchi hizo ili kuwaunganisha katika sekta mbalimbali zikiwamo za uchumi na biashara.

Tabia Maulid Mwita alitoa rai hiyo jana alipofungua kongamano la nchi wanachama wa jumuiya hiyo katika kuadhimisha lugha ya Kiswahili duniani kote katika hoteli ya Golden Tulip, Unguja.

Alisema lugha ya Kiswahili imepiga hatua kubwa katika baadhi ya nchi za jumuiya hiyo huku ikitumika katika kuongeza utenganifu wa shughuli mbalimbali zikiwamo za kibiashara, utamaduni na kijamii.

Alisema huu ni wakati mwafaka wa kuona Kiswahili kinapiga hatua kubwa katika masuala ya kibiashara na kuinua uchumi kwa nchi wanachama wakati wanapofanya shughuli zao ikiwamo katika maeneo ya mipakani.

"Huu ni wakati mwafaka kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kuona tunaitumia lugha hiyo katika kuongeza utenganifu katika sekta mbalimbali zikiwamo za kibiashara kwa maslahi ya wananchi wetu," alihimiza.

Waziri huyo pia alivitaka vyombo vya habari kukitumia Kiswahili vizuri kwa lengo la kupanua wigo wa lugha hiyo kutumika vizuri na siyo kupotosha.

"Tumeshuhudia vyombo vya habari vikitumia vizuri lugha ya Kiswahili kwa maslahi ya wananchi wetu na kuacha upotoshaji ambao umekuwa ukirudisha nyuma maendeleo ya lugha hiyo," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Stephen Mlote, alisema jumuiya hiyo itahakikisha itatumia muda wake mwingi kuona lugha ya Kiswahili inatumika vizuri, hata kwenye vyombo vya kutunga sheria.

Aliyataja mafanikio yaliyofikiwa katika kukiendeleza Kiswahili ni pamoja na kuwaunganisha wananchi wake katika shughuli za kibiashara katika maeneo ya mipakani ambapo lugha hiyo inatumika kikamilifu katika kukuza uchumi.

"Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kazi yetu kubwa kuhakikisha lugha ya Kiswahili inatumika vizuri kwa ajili ya kuwaunganisha nchi wanachama katika sekta mbalimbali zikiwamo za biashara na utamaduni," alisema.

Kaimu Katibu Mkuu Mtendaji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki (KAKAMA), James Jowi, alisema taasisi yake inaendelea na malengo yake makubwa ambayo ni kuratibu na kusimamia kazi za mabaraza ya Kiswahili ya kitaifa na asasi zingine wanachama.

Alisema wataendelea kufanya kazi za utafiti wa kikanda na kuzisaidia nchi wanachama kuanzisha vituo vya elimu ya juu na utafiti katika Kiswahili.

"Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ndiyo walioanzisha taasisi hii, tunaendelea na majukumu yetu kuona lugha hii inakuwa miongoni mwa lugha kubwa duniani na kutumika katika maeneo yote muhimu ikiwamo biashara," aliahidi.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akisalimiana na Balozi wa Tanzania nchini Indonesia, Macocha Yembele alipofika ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar kwa ajili ya kujitambulisha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Zanzibar yaahidi ushirikiano Indonesia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Zanzibar itaendeleza ushirikiano na Indonesia katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

Alitoa aahidi hiyo jana ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar katika mazungumzo yake na Baozi wa Indonesia, Macocha Yembele.

Makamu wa Rais alisema serikali inategemea mafanikio katika kukuza uchumi wa Tanzania kupitia ushirikiano uliopo baina ya nchini hizo mbili.

Hemed alisema Zanzibar ina uhusiano mkubwa hasa wa kibiashara na Indonesia katika bidhaa ya karafuu, akimwomba balozi huyo kuongeza ushirikiano na wakulima wa zao hilo ili kujua njia bora wanazotumia katika kuzalisha zao hilo kwa wingi.

Pia alimwomba balozi huyo kuitangaza Sera ya Zanzibar ya Uchumi wa Buluu hasa ikizingatiwa kuwa Indonesia ina visiwa vingi mithili ya Zanzibar.

Hemed alitumia fursa hiyo kumwomba Balozi huyo kuitangaza Tanzania kwa mazuri yake hasa utalii na vivutio mbalimbali vilivyoko nchini ili kuikuza sekta ya utalii.

"Nikuombe ueleze fursa za uwekezaji zilizoko hapa Zanzibar na kuwakaribisha wawekezaji kutoka Indonesia kuja kuwekeza ili kuzidisha zaidi uhusiano na udugu uliopo baina ya nchi zetu mbili," alisema.

Balozi wa Indonesia, Macocha Yembele, alisema atasimamia maombi ya viongozi wakuu katika kuiwakilisha Tanzania kwenye majukumu yake ikiwamo kuongeza diplomasia na kuzitangaza fursa mbalimbali za kiuchumi zilizoko Tanzania.

# Mchanga, kokoto zaingiza mabilioni

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imekusanya Sh. bilioni tatu katika kipindi cha miezi mitatu kutokana na mauzo ya maliasili zisizorejesheka ikiwamo kifusi, mchanga, mawe, kokoto na vumbi.

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Mngerza Mzee Miraji, alibainisha hayo jana wakati akimkabidhi ofisi Katibu Mkuu mpya, Joseph John Kilangi, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Dk. Mngereza alisema kutokana na tatizo la upotevu wa maliasili, kwa kushirikiana na watendaji wake waliamua kuchukua hatua za makusudi kuanzisha mfumo wa kudhibiti maliasili zisizorejesheka ili kuzuia upotevu wa mali hizo.

"Kutoka Aprili hadi Juni mwaka huu, wizara imeweza kuingiza fedha hizo ambapo mwezi wa Juni pekee uliingiza Sh. bilioni 1.05.

"Mfumo huo ni mzuri, unaweza kuona gari linapoingia katika shimo la maliasili, mali iliyobebwa, uwezo wa gari na wapi linaelekea, hali ya kuwa nipo ofisini, hata usiku. Pia mtu akilipa malipo benki kupitia mfumo huu, unaonyesha fedha zilizoingia, aina zote za malipo," alisema.

Aliwashukuru watendaji wa wizara hiyo kwa ushirikiano mkubwa waliompa katika kipindi chote alichotumika wizara hiyo, akisisitiza ni hali inayoonyesha dhamira ya serikali katika kuwaletea wananchi wake maendeleo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Kilangi, aliyekabidhiwa dhamana hiyo, alisema anaamini yote aliyokabidhiwa atayaendeleza na kuwaomba watendaji wa wizara hiyo kumpa ushirikiano kama walivyompa Dk. Mngereza kwa kuwa wote wanajenga nyumba moja.

Aliwataka watendaji wa wizara hiyo kutomchoka mapema kutokana na kuwaita mara kwa mara kwa sababu majukumu hayo ni mapya kwake, hivyo anahitaji kujifunza mambo mengi kupitia kwao.

Waziri katika wizara hiyo, Hassan Kaduara, aliwataka watendaji wa wizara hiyo kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya serikali ambayo ni chachu ya maendeleo.

Alisema ukusanyaji mzuri wa mapato ya serikali yanayotokana na rasilimali zilizopo, unatokana na utendaji mzuri wa wafanyakazi, hivyo wanapaswa kuongeza bidiii ili serikali kupiga hatua.

Makabidhiano hayo yamefanyika kufuatia uteuzi aliyoufanya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi Juni 30 mwaka huu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

Nafasi za Kazi ya ualimu, sifa **Diploma au Digrii** masomo ya hesabu na science darasa la 6 na 7 Piga simu kabla ya tarehe 7/7/2022.

**Simu 0783298900**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya BAGAMOYO**
**Kituo cha KEREGE Mkoa Wa PWANI**
**Shauri la madai / ndoa na 27/2022**
**Jina la Mdai ZUBEDA SAIDI MKANDE**
**Jina la Mdaiwa ALPHONCE WILLBARD MKAMA**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu za madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa ALPHONCE WILLBARD MKAMA**
**Kwa kuwa mdai / wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba ( Eleza hapo habari za mdai )**

**KUJIBU MADAI.**
Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe ......mwezi ..... mwaka 2022 saa2.30 Asubuhi kwa mujibu wa madai haya na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mahsahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juuu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakamani inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
**Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 23 mwezi 6 mwaka 2022.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KEREGE - BAGAMOYO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

### KUITWA SHAURINI SHAHIDI

**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA MWANZO MIKONGENI**
**WILAYA YA MVOMERO**
**MADAI NAMBA 10...2022**
**MDAI: HERENA D/O MBAGA**
**MDAIWA: MKOI S/O GICHOGO**
**KWA: MKOI S/O GICHOGO**
**MKAZI WA MANGAE**

Kwa kuwa mdai / wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba ( Eleza hapo habari za mdai ) **KWA AJILI YA MADAI YA TSH.1600,000/=UNAZODAIWA.**

Kwa hiyo nahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya jumatatu tarehe 11 mwezi 07 mwaka 2022 saa2.30 Asubuhi/alasiri kwa mujibu.Madai hayo,na kuwa siku hiyo siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta maashahidi wako/wetu na hati zote zinahusu shauri hilo kwajili ya kujitetea katika shauri hilo
**ANGALIA** Kama hukuhudhuria/hamkuhuzuria siku iliyotajwa hapo juuu.Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shauri hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
**Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 27/06/2022.**

Hakimu wa Mahakama ya

**Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MIKONGENI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALEHE LIANA MMBAGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye usajili namba **T129BAG, CHASSIS NAMBA : SXU100004618** na **ENGINE NAMBA: 1ZMNIL.**

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/268319/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA HAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 42...2022**
**MDAI: PETER FRANCIS GUNI**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: PATHEC LTD (THECLA KALAGE)**
**KWA: THECLA KALAGE**

### POPOTE ULIPO

**OMBI LA MDAI: PETER FRANCIS GUNI**
**MADAI YA PESA THS.11, 000,000/=GHARAMA TSH.15000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo **tarehe 11 mwezi 07 mwaka 2022 saa2.30 Asubuhi.**
Angalia Kama hukuhudhuria/hamkuhuzuria siku iliyotajwa hapo juuu.Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini ,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa kuhudhuria bila sababu.
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **tarehe 05/07/2022.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

## NKAYA COMPANY LIMITED

### MARUDIO YA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**NOTISI YA KULIPA DENI NDANI YA SIKU SABA [7], AU MALI ILIYOWEKWA KAMA DHAMANA ITAUZWA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **KCB BANK TANZANIA,** mdaiwa wa dhamana ifuatayo anatakiwa alipe deni lake ndani ya siku **SABA [7]** kutokea tarehe ya kutoka kwa hili tangazo.
Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kuuzwa kwa mali aliyo iweka kama dhamana.

| MAELEZO KUHUSU DHAMANA | USAJILI WA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE NA MUDA |
|---|---|---|---|
| KIWANJA CHENYE JENGO KUBWA LA KUHIFADHIA MIZIGO PAMOJA NA OFISI | CT NO. 1169, LO NO. 44116 KIWANJA NAMBA 6/8, KITALU "C" | ILIYOPO ENEO LA UNGALIMITED JIJINI ARUSHA. | 16/07/2022 SAA 03:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na asilimia 75% atatakiwa kumaliza ndani ya siku kumi na nne (14) endapo atashindwa kulipa kwa muda huo uliowekwa, pesa aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa.
2. Ukaguzi wa dhamana zinazofanyiwa mnada utafanyika siku ya mnada.
3. Gharama za kuhamisha mali au kumtoa mtu ndani pamoja na kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe.
4. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
5. Endapo yeyote atajitokeza kuharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kulazimika kulipa gharama za mnada.
6. Dalali wa mnada ni Nkaya Company Limited ndio wenye mamlaka na maamuzi ya mwisho ya kumtangaza mshindi.

**NKAYA MOB: 0626180070, 0717208108, 0788448341, 0753000825**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Russia yateketeza makombora ya Marekani

**MOSCOW,** Russia

WIZARA ya Ulinzi ya Russia, jana imetangaza kuteketeza makombora mawili ya HIMARS MLRS yaliyotolewa na Marekani kama msaada kwa Ukraine.

Msemaji wa Wizara hiyo, Luteni-Jenerali Igor Konashenkov, alidai makombora hayo yaliyotengenezwa na Marekani ya HIMARS yaliharibiwa sambamba na maghala mawili ya kuhifadhi risasi katika jimbo la Donbas

Shambulio hilo lilifanywa kwa kutumia makombora yenye usahihi wa hali ya juu ya Russia karibu na kijiji cha Malotaranovka katika Jamhuri ya Watu wa Donetsk kama ilivyojiita.

Hata hivyo, mshauri wa Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ukraine, Anton Gerashchenko, alikana taarifa za jeshi la Russia kuhusu uharibifu wa makombora ya HIMARS yaliyopelekwa Ukraine kutoka Marekani.

**Mashambulizi ya makombora ya Russia yameteketeza soko kuu katika mji wa Sloyansk mashariki mwa Ukraine, na kuua watu wawili na wengine saba wamejeruhiwa.**

Data ya jeshi la Russia pia imekataliwa na mbunge wa Ukraine, ambaye ni mwanachama wa kundi la Umoja wa Ulaya Oleksiy Goncharenko.

**ULAYA YAONYA UWEPO WA HALI MBAYA**

Rais wa Halmashauri Kuu ya Ulaya, Ursula von der Leyen, ameonya kuwa Umoja wa Ulaya unahitaji kuweka mipango ya dharura kujiandaa kwa kusitishwa kabisa kwa gesi kutoka Russia.

Von der Leyen ameliambia bunge la Ulaya mjini Strassbourg, nchini Ujerumani kuwa baadhi ya nchi wanachama tayari zimeathirika kutokana na Russia kupunguza au kukatwa kabisa kwa gesi wakati ukiendelea mkwamo wa kisiasa kuhusu uvamizi nchini Ukraine'.

Umoja wa Ulaya tayari umeiwekea Russia vikwazo, ikiwa ni pamoja na nishati ya mafuta na gesi, na kuwa na mpango wa kuachana na bidhaa zinazodhitibiwa na serikali ya nchi hiyo.

Nchi za umoja huo tayari zilikubaliana mwezi uliopita kuwa hifadhi ya gesi yote asilia katika jumuiya hiyo yenye nchi wanachama 27 inapaswa kujazwa hadi karibu asilimia 80 kwa ajili ya msimu ujao wa baridi ili kuepusha uhaba wakati wa msimu huo.

**MAKOMBORA YATEKETEZA SOKO SLOYANSK**

Mashambulizi ya makombora ya Russia yameteketeza soko kuu katika mji wa Sloyansk mashariki mwa Ukraine, na kuua watu wawili na wengine saba wamejeruhiwa.

Mkuu wa Mkoa wa Donetsk, Pavlo Kyrylenko alisema tukio hilo sawa na ugaidi.

Meya Vadym Lyakh, alisema Sloviansk ilikuwa ikishambuliwa na askari wa Russia kutoka maeneo ya karibu, kwani inakuwa jiji la mstari wa mbele.

Alichapisha picha za moto huo kwenye mtandao wa Facebook, akielezea kuna mashambulizi makubwa ya makombora, na kuwataka watu kusalia kwenye makazi yao.

Russia inatafuta kukamata eneo lote la viwanda la mashariki la Donbas. Eneo hilo linaundwa na mikoa miwili, Luhansk na Donetsk.

Wiki iliyopita, jeshi la Ukraine lilisema lililazimika kuondoka Lysychansk, ngome yake ya mwisho iliyosalia huko Luhansk, kuepuka mashambulizi makali ya Russia.

Ilisema wanajeshi wake sasa wanaimarisha ngome ili kulinda maeneo inayoshikilia Donetsk, ikiwamo mji wa Sloviansk.

Mkuu wa Mkoa wa Luhansk Serhiy Haidai, alisema Jumanne kwamba mapigano makali yanaendelea kwenye ukingo wa mkoa wa Luhansk karibu na Lysychansk.

Haidai alisema Warusi walikuwa wakiendelea kusababisha hasara. **BBC**



Waumini wa Kiislamu wakinunua mikate kutoka kwa mchuuzi wakati wakisubiri kuanza kwa ibada ya Hija katika mji wa Makka jana. **PICHA: REUTERS**

## Waumini wa kiislamu waanza Ibada ya Hija

**MAKKA,** Saudi Arabia

WAUMINI wa kiislamu wanashiriki ibada ya Hija tangu kuzuka kwa janga la Corona.

Maelfu ya waumini walianza ibada hiyo jana, wengi wao wakiwa bila ya barakoa walianza kumiminika katika eneo takatifu la dini ya Kiislamu, Makka nchini Saudi Arabia. Waislamu milioni moja waliochanjwa, wakiwamo 850,000 kutoka mataifa ya kigeni, waliruhusiwa kushiriki katika hija ya mwaka huu, ikiwa ni tofauti na ilivyokuwa miaka miwili iliyopita wakati idadi hiyo ilipunguzwa kutokana na janga la corona.

Mwaka 2019, waumini milioni 2.5 wa Kiislamu kutoka ulimwenguni kote walishiriki katika ibada hiyo ya Hija inayoandaliwa kila mwaka, ambayo ni nguzo ya mwisho kati ya tano za imani ya kiislamu. **DW**

## Katibu Mkuu OPEC afariki ghafla

**ABUJA,** Nigeria

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi duniani (OPEC), raia wa Nigeria Mohammed Barkindo, amefariki dunia ghafla akiwa na umri wa miaka 63.

Kifo hicho kimetangazwa na ofisa mkuu mtendaji wa Shirika la Mafuta la Nigeria (NPC), Mele Kyari, ambaye alisema Barkindo alifariki dunia saa tano jana usiku. Hakutoa maelezo kuhusu mazingira ya kifo chake. Barkindo alikuwa nyumbani kwake Nigeria kwa ajili ya mkutano wa kilele wa nishati mjini Abuja, na alikutana na kuzungumza na Rais Muhammadu Buhari juzi.

Wakati wa mkutano huo alitoa hotuba inayoonya kuwa sekta ya mafuta na gesi ulimwenguni iko hatarini. Alitarajiwa kukabidhi wadhifa huo kwa Haitham Al Ghais wa Kuwait Agosti mwaka huu.

Tangu alipochokua nafasi hiyo ndani ya OPEC mwaka 2016, Barkindo aliongoza katika nyakati ngumu kwa muungano huo wa wazalishaji mafuta, ambao zilishuhudia masoko yakiyumba kutokana na matukio ya kihistoria kama vile COVID-19, kutengenezwa kwa muungano wa OPEC+ uliofanywa na Russia na mataifa mengine yasiyo ya OPEC, na hivi sasa uvamizi wa Russia nchini Ukraine. **DW**

## Msafara wa rais Nigeria washambuliwa

**LOGOS,** Nigeria

WATU wenye silaha wameushambulia msafara wa Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari katika eneo la Katsina, analotoka kiongozi huyo.

Katika tukio hilo, watu wawili walipata majeraha ambao walikuwa katika msafara wa awali wa walinzi, maofisa wa itifaki na vyombo vya habari.

Taarifa kutoka kwa msemaji wa rais, Garba Shehu, msafara huo ulikuwa umetangulia kabla ya rais Buhari kuwasili katika mji wake wa Daura kusherehekea sikukuu ya Eid-ul-Adha mwishoni mwa wiki. Washambuliaji hao walipofyatulia risasi magari hayo, lakini wanajeshi walijibu na kuwazuia na shambulizi hilo.

Katsina ni mojawapo ya majimbo ya kaskazini-magharibi mwa Nigeria yaliyoathiriwa na vitendo vya uhalifu wa majambazi.

Watu wengi wameuawa na maelfu kutekwa nyara katika eneo hilo tangu 2015. **BBC**

# SAKHO, MWEZI MMOJA ATWAA TUZO MBILI BARA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Pape Sakho amefanikiwa kutwaa tuzo mbili katika kipindi cha Juni baada ya kuchaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa mwezi huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara lakini akishinda tuzo nyingine inayotolewa na mashabiki wa klabu hiyo.

Sakho, ambaye ana msimu mmoja tu tangu asajiliwe na klabu hiyo akitokea Teungueth ya Senegal alichaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa mwezi huo na Kamati ya Tuzo ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwenye kikao kilichofanyika Julai 4, mwaka huu.

**Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi, mchezaji hiyo ali chaguliwa baada ya kuonyesha kiwango kizuri mwezi huo, aki funga mabao manne na kuhusika na magoli mengine matatu ka tika dakika 222 za mechi tatu al izoichezea timu yake ya Simba.**

Taarifa hiyo ilisema, Simba ilicheza mechi tano mwezi huo, ikishinda tatu, sare moja na kupoteza moja, mchezaji huyo akiwashinda Idris Mbombo wa Azam FC, na Shiza Kichuya wa Namungo FC ya mkoani Lindi.

Wakati Kamati ya Bodi ya Ligi ikimchagua kuwa mshindi wa tuzo hiyo kwa Juni, Sakho pia amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi huo huo wa mashabiki wa klabu yake.

Kwa mujibu wa taarifa ya Simba, mashabiki walimchagua kuwa mchezaji bora baada ya kupata kura nyingi dhidi ya wachezaji wenzake ambao ni Peter Banda, raia wa Malawi na Mtanzania Kibu Denis.

Kama ilivyo kwa tuzo ya mchezaji bora wa ligi, tuzo ya wachezaji kutoka kwa mashabiki wa Simba nayo hutolewa kila mwezi kwa mchezaji ambaye ameonekana kufanya vyema kwa mwezi huo.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, ameibuka kuwa kocha bora wa mwezi huo.

Kocha huyo aliwabwaga Nasreddine Nabi wa Yanga ambaye timu yake ilichukua ubingwa na Fred Minziro wa Geita Gold, aliyemaliza msimu akiwa katika nafasi ya nne.

Sherehe za tuzo zinazotolewa na TFF zinatarajiwa kufanyika leo jijini Dar es Salaam.



Mwanahabari, Prisca Kishamba (kushoto), akimkabidhi fedha Sh. milioni 2.5 straika mpya wa Azam FC, Abdul Suleimani 'Sopu' kama zawadi baada ya kuonyesha kiwango kizuri katika mashindano ya Kombe la FA ambapo nyota huyo aliifungia timu yake ya zamani, Coastal Union mabao matatu kwenye mechi ya fainali na kufikisha magoli tisa katika michuano hiyo iliyomalizika Jumamosi iliyopita jijini Arusha. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Dodoma Jiji kusajili wapya 10

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Dodoma Jiji umesema unatarajia kusajili wachezaji wapya 10 kwa ajili ya kuboresha kikosi chao kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaoanza Agosti 17, mwaka huu, laniki ikitangaza kuendelea na kocha wake mkuu, Mrundi Masoud Djuma.

Katibu Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Fortunatus John, amesema baada ya kumalizika kwa ligi wamepata mapendekezo kutoka kwa benchi la ufundi la kuacha idadi hiyo ya wachezaji na kuhitaji kusajili wengine ambao watakiongezea nguvu kikosi hicho.

John alisema anahitaji kuona timu yao inavuna matokeo chanya katika msimu ujao na kufikia malengo yao mapema badala ya kupambana kujinusuru kutoshuka daraja.

"Malengo yetu msimu huu uliomalizika hayakutimia baada ya kukutana na changamoto kadhaa kwenye ligi. Tumekubaliana kuendelea na walimu hawa waliopo ambao wametupa mapendekezo ya kuwaacha nyota kadhaa na kuleta maingizo mapya, hivyo mawindo bado yanaendelea," alisema John.

Katibu huyo alisema pia wameanza kuwaongezea mikataba wachezaji ambao wanahitaji kuendelea nao akimtaja mmoja wao ni nahodha, Mbwana Kibacha ambaye ataendelea kusalia kwenye klabu hiyo baada ya kuongezewa kandarasi.

Katika hatua nyingine, katibu huyo alisema tayari wameanza mchakato wa kujenga hosteli pamoja na kiwanja cha mazoezi kwa ajili ya kuongeza ufanisi kwenye kikosi hicho.

"Tunafanya hivyo ili tuwe na sehemu yetu wa kambi itakayowaweka kwenye hali ya usalama zaidi na kuwalinda wachezaji wetu ili viwango vyao visishuke," aliongeza ofisa huyo.

## Msajili Zanzibar aziamsha klabu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MSAJILI wa Vyama vya Michezo Zanzibar, Abubakar Lunda, amesema ofisi yake imejipanga kuchukua hatua kwa timu na vyama vya michezo ambavyo havitalipa ada kama iliyoelekezwa kwa mujibu wa sheria, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lunda alisema vipo baadhi ya vilabu na vyama vinaendesha mashindano bila ya kufuata Sheria za Baraza la Michezo la Zanzibar (BMZ), hasa katika masuala ya usajili kila inapofika msimu mpya wa mashindano.

Lunda ofisi yake ina uwezo wa kuvifutia usajili vyama au vilabu vitakavyoshindwa kulipa ada inayotakiwa kwa kipindi cha mwaka mmoja.

"Vipo baadhi ya vilabu na vyama havioni umuhimu wa kulipa ada, hii ni kinyume cha sheria ya usajili wa vyama hivyo katika ofisi ya mrajisi, na upo uwezo wa kuvifutia usajili endapo watashindwa kulipa kwa mwaka mmoja au msimu mmoja," Lunda alisema.

Aliongeza ofisi yake imeandaa mkakati wa kufanya ziara kwa vyama vya michezo vyote kuanzia ngazi ya taifa, mikoa na wilaya ili kutoa elimu itakayowasaidia kupata uelewa wa sheria ya usajili na umuhimu wake.

Alitaja kiasi kinachotakiwa kulipa kwa mwaka kwa klabu au chama ni Sh. 10,000 tu.

## Tanzania kuchuana kikapu U-18 Afrika

**Na Shufaa Lyimo**

TANZANIA imepata nafasi ya kushiriki fainali za 23 za vijana wa umri chini ya miaka 18 za mchezo wa kikapu Afrika zinazotarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 4 hadi 14, mwaka huu nchini Madagascar.

Rais wa Shirikisho la Kikapu Nchini (TBF), Michael Kadebe, alisema Tanzania imepata nafasi hiyo baada ya kufanya vizuri katika mashindano ya Kanda ya Tano yalifanyika Juni 13 hadi 18, mwaka huu nchini Uganda.

"Washindi watakaopatikana katika mashindano hayo ya Afrika watapata nafasi ya kwenda kushiriki michuano ya Kombe la Dunia ambayo itafanyika mwakani," alisema Kadebe.

Rais huyo alisema anaamini kupitia mashindano hayo watapata wachezaji wazuri ambao watakwenda kuiwakilisha vyema nchi kwenye fainali za dunia.

Aliongeza kwa kuiomba serikali iendelee kuwaunga mkono ili waende kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika fainali hizo za Afrika.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POGBA, JUVE KIMEELEWEKA**

JUVENTUS wamefikia makubaliano ya kumnunua tena kiungo wa kati, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, kwa mkataba wa miaka minne baada ya mkataba wake wa sasa na Manchester United kumalizika. ***(Sky Sports)***

**CHELSEA KUSAJILI WAPYA**

CHELSEA wanatumaini kukamilisha usajili wa wachezaji wawili wanaolengwa wiki hii, huku mazungumzo yakiendelea kuhusu wachezaji wa kimataifa wa Uholanzi, Matthijs de Ligt wa Juventus mwenye umri wa miaka 22, na Nathan Ake wa Manchester City (27). ***(Standard)***

**DE LIGT, BAYERN WATETA**

BAYERN Munich wamefikia makubaliano ya mdomo na Matthijs De Ligt kutaka kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Sport1)***

**NEWCASTLE MAMBO MAGUMU**

KLABU ya Newcastle haiko tayari kufikia bei ya Bayer Leverkusen ya pauni milioni 60 kwa winga wa kimataifa wa Ufaransa, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

**TORRES KUTUA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur imeonyesha nia ya kumsajili mlinzi wa kimataifa wa Hispania na Villarreal, Pau Torres mwenye umri wa miaka 25, licha ya kukaribia kuwasili kwa mlinzi wa kati wa Ufaransa, Clement Lenglet (27) kutoka Barcelona. ***(Mirror)***

**SOLOMON ANUKIA FULHAM**

FULHAM wanakaribia kumsajili winga wa kimataifa wa Israel, Manor Solomon mwenye umri wa miaka 22 kwa mkopo kutoka Shakhtar Donetsk. ***(Athletic)***

**BRENTFORD YAJIPANGA**

KLABU ya Brentford inatarajia kuthibitisha usajili wa pauni milioni 18.9 wa beki wa kimataifa wa Scotland, Aaron Hickey mwenye umri wa miaka 20, kutoka Bologna wiki hii. ***(Guardian)***

**RICHARDS KUTUA FOREST**

KLABU ya Nottingham Forest imefanya mazungumzo na Bayern Munich ili kumsajili beki wa kushoto wa England, Omar Richards mwenye umri wa miaka 24, ambaye anapatikana kwa pauni milioni 8.5. ***(Telegraph via Nottingham Post)***

**POCHETTINO KUREJEA EPL**

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, 50, anatazamia kurejea katika Ligi Kuu England maarufu EPL baada ya kutimuliwa na Paris Saint-Germain.

**ARINO AKARIBIA SOUTHAMPTON**

KLABU ya Southampton ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kimataifa wa Nigeria, Joe Aribo, 25, kutoka Rangers kwa pauni milioni 10. ***(Athletic)***

**KOKCU KUTUA LEICESTER**

KLABU ya Leicester imeanza mazungumzo na Feyenoord kuhusu kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Uturuki, Orkun Kokcu, 21. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HATIMAYE NEYMAR SASA KUBAKIA PSG

**Ni taarifa kutoka kwa kocha mpya wa timu hiyo ambaye ameweka wazi...**

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA mpya wa Paris Saint-Germain, Christophe Galtier, amekiri anatumaini Neymar atasalia hapo Parc des Princes zaidi ya msimu huu wa joto.

**Nyota huyo wa Brazil anatajwa ana mipango ya kuondoka katika klabu hiyo mwezi huu, huku Manchester United, Manchester City, Chelsea na Newcastle United zote zikimwania.**

Bayern Munich, Juventus na AC Milan pia zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili Neymar, lakini hadi sasa hakuna aliyetuma ofa.

Kwa mujibu wa 90min, PSG hawajashawishika na wazo la kumuuza Neymar msimu huu wa joto, ingawa wapo tayari kusikiliza ofa.

Wakati wa utambulisho wake, Galtier aliulizwa maoni yake ni nini kwa Neymar kikosini, na hakuficha nia yake ya kutaka kumbakiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

"Ni kocha gani ambaye hatapenda kuwa na Neymar kwenye kikosi chake?" Alisema Galtier akiwaambia waandishi wa habari. "Ni mchezaji wa kiwango cha dunia.

"Hakika, unahitaji usawa, lakini nina wazo la jinsi ninatakavyomtumia. Natumaini atakaa nasi."

Galtier pia alikiri furaha yake ya kufanya kazi na Kylian Mbappe, ambaye alitia saini mkataba mpya na PSG mapema mwezi huu, lakini akasisitiza mafanikio yoyote ambayo klabu itafurahia yatakuwa juhudi za timu, badala ya kutokana na nyota yoyote wa mbele.

"Kama kocha wa Ufaransa, nilifurahi sana Kylian amebaki," alisema Galtier. "Ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani.

"Najua anachotarajia kutoka kwa timu yake. Tunajua uwezo wake na umuhimu alionao. Ikiwa watu hawa wakuu watafurahi kufanya kazi pamoja, PSG watakuwa na msimu mzuri. Natumaini timu itakuwa bora kama ilivyokuwa msimu uliopita."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,012,7
MECHI KALI
SOCHI
VERSUS
CSKA MOSCOW
1 | 2.74
X | 3.53
2 | 2.21
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JORGINHO HATAKI KUONDOKA CHELSEA



**LONDON,** England

WAKALA wa kiungo wa Chelsea, Jorginho amesisitiza kipaumbele cha Mtaliano huyo ni kujadili mkataba mpya pale Stamford Bridge.

Jorginho ameingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na 90min inaeleweka The Blues hao wana furaha kumuuza msimu huu wa joto huku kukiwa na nia ya kocha wa zamani, Maurizio Sarri, ambaye sasa yuko Lazio, pamoja na Juventus.

Kuvutiwa na Turin kumesababisha tetesi kuwa Jorginho anaweza kutumika katika kubadilishana fedha na beki wa kati Matthijs de Ligt, ambaye anavutiwa sana na kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel.

Hata hivyo, kwa mujibu wa wakala wa Jorginho, Joao Santos, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 hafikirii kurejea Italia kwa sasa.

"Chelsea ndio kipaumbele," alisema Santos akiiambia TuttoMercatoWeb.

"Mkataba wake utaisha mwaka 2023. Nadhani tutazungumza kuhusu kuongezwa upya kuanzia Septemba."

Licha ya maoni ya Santos, 90min inaelewa Chelsea bado wako tayari kusikiliza ofa kwa Jorginho huku Tuchel akitazama kujenga upya safu yake ya kiungo.

N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 31 pia amebakiza miezi 12 kukamilika kwa mkataba wake na vyanzo vimethibitisha Chelsea hawana mpango wa kuwabakisha wachezaji wote wawili hadi 2023, huku mazungumzo yakiendelea kuhusu mustakabali wao.



## *United yakamilisha usajili wa Malacia*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imemsajili beki wa pembeni, Tyrell Malacia kutoka Feyenoord kwa mkataba wa miaka minne hadi Juni mwaka, 2026 akiwa na chaguo la kuongeza mwaka mmoja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 22, atagharimu euro milioni 15 na euro milioni mbili zaidi katika nyongeza.

Malacia, ambaye aliichezea Feyenoord mechi 136, ni ujio mpya wa kwanza wa kocha, Erik ten Hag ambaye ametua hapo akitokea Ajax.

Malacia aliongeza: "Hii ni sura mpya kwangu, ligi mpya na wachezaji wenzangu wapya na kocha mzuri anayetuongoza.

"Ninajua kutokana na kucheza dhidi ya timu zake kwenye Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, sifa alizonazo na kile anachodai kutoka kwa wachezaji wake.

"Wakati najua bado ni mdogo na nitaendelea kujiendeleza, ninaweza kuwaahidi mashabiki wa United nitafanya kila kitu uwanjani kila nitakapovaa jezi nyekundu."

Beki huyo wa upande wa kushoto alikuwa akifanya mazungumzo na klabu ya Lyon ya Ufaransa kabla ya United kuingilia mchakato huo.

798,111/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE


| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/07/22 | 22:30 | Criciuma SC vs Vasco da Gama | 2.53 | 2.82 | 3.12 |
| 02. 10/07/22 | 00:30 | Sampaio MA vs Ituano SP | 2.47 | 2.98 | 3.03 |
| 03. 10/07/22 | 02:00 | Charlotte FC vs Nashville | 2.45 | 3.22 | 2.97 |
| 04. 10/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs New York Red Bulls | 2.92 | 3.57 | 2.31 |
| 05. 10/07/22 | 02:30 | Goias vs Atletico Pr | 2.89 | 3.08 | 2.54 |
| 06. 10/07/22 | 03:30 | Houston Dynamo vs Dallas | 2.36 | 3.47 | 2.92 |
| 07. 10/07/22 | 08:00 | Consadole Sapporo vs Kashima Antlers | 2.89 | 3.34 | 2.47 |
| 08. 10/07/22 | 13:00 | Sagan Tosu vs Kashiwa Reysol | 2.32 | 3.23 | 3.23 |
| 09. 10/07/22 | 13:00 | Omiya Ardija vs Tokyo Verdy | 2.71 | 3.32 | 2.56 |
| 10. 10/07/22 | 13:00 | Oita Trinita vs Fagiano Okayama | 2.47 | 3.00 | 3.10 |
| 11. 10/07/22 | 13:00 | Avispa Fukuoka vs Kyoto Sanga | 2.62 | 2.97 | 3.02 |
| 12. 10/07/22 | 13:00 | Suwon City vs FC Seoul | 2.90 | 3.35 | 2.42 |
| 13. 10/07/22 | 16:00 | Utsiktens BK vs Osters IF | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 14. 10/07/22 | 16:00 | Seinajoen JK vs Honka | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 15. 10/07/22 | 19:00 | Sandefjord vs Aalesunds | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 16. 10/07/22 | 02:30 | CA Platense vs Newell'S Old Boys | 2.62 | 3.07 | 2.92 |
| 17. 10/07/22 | 22:00 | Corinthians vs Flamengo | 2.73 | 3.08 | 2.68 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 07/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 2389 | Shanghai Shenhua vs Hebei Zhongji | 1.19 | 5.71 | 11.81 |
| 12:30 | 4843 | Beijing Guoan vs Meizhou Kejia | 2.60 | 3.18 | 2.50 |
| 14:30 | 1066 | Henan Jianye vs Guangzhou RF | 1.19 | 5.71 | 11.81 |
| 14:30 | 4096 | Shijiazhuang vs Shenzhen | 2.94 | 3.14 | 2.27 |
| 15:00 | 5786 | Comoros vs Botswana | 4.13 | 3.05 | 1.89 |
| 17:30 | 2798 | Faisaly Amman vs Shabab Al Ordun | 1.57 | 3.73 | 5.11 |
| 18:00 | 1442 | Jazeera Amman vs AL Salt | 2.56 | 3.15 | 2.56 |
| 18:00 | 1631 | Angola vs Seychelles | 1.23 | 5.09 | 10.77 |
| 18:00 | 5755 | Alashkert Martuni vs Hamrun Spartans | 1.35 | 4.92 | 8.04 |
| 19:00 | 1158 | Flora Tallinn vs Seinajoen JK | 2.13 | 3.49 | 3.18 |
| 19:00 | 1996 | Grorud IL vs Sandnes Ulf | 2.51 | 3.39 | 2.46 |
| 19:00 | 2635 | Stabaek vs Stjordals-Blink | 1.18 | 6.08 | 11.76 |
| 19:00 | 2742 | Raufoss vs Mjondalen | 2.15 | 3.39 | 2.94 |
| 19:00 | 3190 | Bryne vs Kongsvinger IL | 1.91 | 3.60 | 3.35 |
| 19:00 | 3510 | Ranheim vs Skeid Fotball | 1.51 | 4.23 | 4.92 |
| 19:00 | 3560 | Saburtalo Tbilisi vs Partizani Tirana | 2.38 | 3.24 | 2.93 |
| 19:00 | 3605 | Kristiansund vs Tromso | 3.02 | 3.37 | 2.24 |
| 19:00 | 3648 | PPJ vs FC Futura | 1.49 | 4.61 | 4.71 |
| 19:00 | 3754 | Aasane Fotball vs Kfum Oslo | 2.95 | 3.49 | 2.11 |
| 19:00 | 3862 | Pogon Szczecin vs KR Reykjavik | 1.19 | 6.26 | 14.13 |
| 19:00 | 3991 | FK Panevezys vs Milsami Orhei | 2.02 | 3.43 | 3.53 |
| 19:00 | 4083 | KuPS Kuopio vs Dila Gori | 1.48 | 4.44 | 5.85 |
| 19:00 | 5079 | IK Start vs Brann | 3.83 | 3.83 | 1.73 |
| 19:00 | 5467 | FC Jazz vs Grankulla Ifk | 1.60 | 4.54 | 3.94 |
| 19:00 | 5596 | Sogndal vs Fredrikstad | 2.17 | 3.48 | 2.84 |
| 19:30 | 5803 | Ruzomberok vs Zalgiris Kaunas | 1.32 | 5.22 | 8.44 |
| 20:00 | 1368 | Sfintul Gheorghe vs NK Mura | 3.29 | 3.44 | 2.10 |
| 20:00 | 1430 | Olimpija Ljubljana vs Differdange | 1.29 | 5.44 | 9.06 |
| 20:00 | 5063 | Dinamo Tbilisi vs Paide Linnameeskond | 1.26 | 5.68 | 10.14 |
| 20:00 | 5340 | Floriana vs Petrocub | 4.13 | 3.78 | 1.77 |
| 20:00 | 5390 | Wydad Casablanca vs Raja Casablanca | 2.42 | 2.79 | 3.04 |
| 20:00 | 5883 | Sochi vs CSKA Moscow | 2.74 | 3.53 | 2.21 |
| 21:00 | 1464 | Bala Town vs Sligo Rovers | 2.54 | 3.35 | 2.64 |
| 21:00 | 1679 | HB Torshavn vs Newtown AFC | 1.83 | 3.62 | 4.03 |
| 21:00 | 4041 | Laci vs Iskra | 1.63 | 3.98 | 4.84 |
| 21:00 | 4348 | Shkendija vs Ararat Yerevan | 2.06 | 3.53 | 3.33 |
| 21:00 | 4803 | KF Gjilani vs FK Liepaja | 3.70 | 3.65 | 1.90 |
| 21:00 | 5086 | Fola vs SP Tre Fiori | 1.31 | 5.24 | 8.66 |
| 21:00 | 5285 | Gremio Novorizontino SP U20 vs Guarani SP U20 | 1.95 | 3.44 | 3.39 |
| 21:15 | 2425 | Lechia Gdansk vs Akademija Pandev | 1.11 | 7.69 | 24.28 |
| 21:30 | 2293 | Dunajska Streda vs Cliftonville Belfast | 1.32 | 4.94 | 9.07 |
| 21:30 | 4290 | Buducnost vs KF Llapi | 1.85 | 3.64 | 3.94 |
| 21:30 | 5619 | Al Sareeh vs AL Aqaba | 2.75 | 3.24 | 2.34 |
| 21:45 | 1791 | UCD Dublin vs Bohemians FC | 6.08 | 4.22 | 1.43 |
| 21:45 | 1880 | Derry City vs FC Riga | 2.83 | 3.39 | 2.37 |
| 21:45 | 2573 | Tre Penne Galazzano vs FK Sloga Simin Han | 28.24 | 11.09 | 1.06 |
| 22:00 | 1371 | FC Universitario de Vinto vs Bolivar | 4.20 | 3.65 | 1.77 |
| 22:00 | 4972 | Norway W vs Northern Ireland W | 1.04 | 9.87 | 29.61 |
| 22:15 | 3119 | Volsungur vs Magni | 1.30 | 5.51 | 6.70 |
| 22:15 | 5669 | HK Kopavogur W vs Fylkir Reykjavik W | 1.47 | 4.61 | 4.91 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MWAITENDA AAHIDI MAZURI NA UWEKEZAJI MPYA YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

MGOMBEA wa Makamu wa Rais wa Yanga, Suma Mwaitenda, amesema endapo atafanikiwa kuingia madarakani atahakikisha ndoto za kujenga uwanja wa Kaunda zinatimia.

**Yanga inatarajia kufanya uchaguzi keshokutwa na katika nafasi hiyo, Mwaitenda anachuana na Arafat Haji wakati Hersi Said ndiye mgombea pekee wa nafasi ya urais.**

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa kampeni zake katika makao makuu ya Yanga, Mwaitenda alisema kama atapata ridhaa ya wanachama kwenye nafasi hiyo, amejipanga kuona timu za vijana zinakuwa na maendeleo.

Mwaitenda alisema pia 'kichwa hakimuumi' kuona mpinzani wake anaongozana na Hersi na kuongeza anaamini wanachama wa Yanga watafanya uamuzi sahihi kwenye kuchagua kiongozi atakayewafaa.

Aliongeza endapo atachaguliwa atahakikisha katika kipindi cha miaka minne ijayo klabu hiyo inakuwa bora na ya kuigwa ndani na nje ya Afrika.

"Miaka minne ijayo ninaamini klabu ya Yanga itafika mbali kutokana na mipango yangu endelevu niliyowawekea," alisema Mwaitenda.

Mgombea huyo ambaye kwa sasa ni mjumbe wa kamati ya utendaji alikuwa katika uongozi unaomaliza muda alikutana na changamoto mbalimbali ambazo kwa uzoefu alioupata, amejiandaa kuzitatua.

"Endapo nitapata nafasi ya uongozi katika klabu hii ya Yanga nitahakikisha maslahi ya uchumi yanakua ikiwa pamoja na mali za klabu hazihamishiki, nitatafuta wawekezaji ambao watasaidia njia ya upatikanaji wa fedha kirahisi, kutokuwapo na madeni ndani ya klabu yetu pendwa," Mwaitenda alisema.

Aliongeza atahakikisha anakuza thamani ya wachezaji huku pia akipandisha mauzo ya tiketi na vile vile kuuboresha uwanja wa Kigamboni.

"Kwa kuwa nina utaalamu na ujenzi, jengo letu linavyumba vizuri ambavyo nikiviboresha tunaweza kuweka kambi ya wachezaji wetu ili tuepushe gharama za kukodi hoteli kwa ajili ya kambi, " alisema mgombea huyo.



Mchezaji wa timu ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 17 wa Cambiasso (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Simba katika mechi ya Ligi ya U-17 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam jana asubuhi. Simba ilishinda mabao 2-1. **PICHA: TFF**

# *Namungo yaahidi kumbakiza Kichuya*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Namungo FC umesema utahakikisha inawabakiza wachezaji wake waliofanya vizuri katika msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliomalizika akiwamo winga mahiri, Shiza Kichuya na kipa namba moja wa Timu ya Taifa ya Burundi, Jonathan Nahimana.

Nyota hao wawili wamemaliza mikataba yao na Namungo na sasa wanahusishwa kuondoka ndani ya timu hiyo kwa Kichuya akidaiwa kurejea Simba wakati Nahimana anawindwa na Azam FC.

Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu alisema baada ya ligi kumalizika, uongozi umekutana na benchi la ufundi na kupokea mapendekezo yake na kuweka wazi ripoti ya Kocha Mkuu, Honour Janza imewataja nyota hao wako katika mipango yake.

Zidadu alisema kutokana na ripoti hiyo, klabu itahakikisha inakamilisha mazungumzo ya kuwabakisha nyota hao na kuongeza wachezaji wapya watakaoitumikia Namungo katika msimu mpya.

"Kweli wachezaji hao na baadhi wamemaliza mikataba, lakini bado wako katika mipango yetu ya msimu ujao na tunatarajia kuhakikisha wanakuwapo ndani ya timu yetu ili kuimarisha zaidi kikosi kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu na Kombe la FA," alisema mwenyekiti huyo.

Alikiri msimu huu hawakufanya vyema na wanajipanga upya kuhakikisha wanakuwa na kikosi imara kitakachowapa matokeo mazuri katika msimu ujao.

Michezo

Alhamisi Julai 7, 2022

Nipashe



## Hatimaye Neymar kubakia PSG

UKURASA 21



Mshambuliaji wa timu ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 17 ya KMC FC (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Kagera Sugar katika mechi ya Ligi ya U-17 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: TFF**

## Simba: Tumepanga kusajili kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Simba ya jijini Dar es Salaam umesema unaendesha mchakato wa usajili wa wachezaji wapya 'kisasa' na kamwe hautashinikiwa na presha yoyote ya ushindani kama ilivyozoeleka.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema klabu yake itasajili wachezaji wapya kutoka ndani na nje ya Tanzania kwa kufuata mahitaji halisi yaliyopendekezwa na benchi la ufundi si vinginevyo.

Ahmed alisema tayari mchakato huo umeshakamilika kwa asilimia kubwa na muda wa kuwatangaza ukifika watawaweka hadharani.

Alisema wanaamini Simba itakuwa na kikosi imara kwa sababu usajili wao umefanyika kwa umakini ili kufikia malengo ambayo yamechagizwa na uzoefu walioupata kwenye michuano ya kimataifa.

"Kwa wenzetu utambulisho wa wachezaji ni biashara, siku ya utambulisho hurejesha sehemu ya gharama za usajili na mauzo ya jezi, sisi bado hatujafikia huko lakini ni lazima tuanze kidogo kidogo kufanya biashara na wachezaji," Ahmed alisema.

Aliongeza pia klabu yake imeandaa utaratibu mzuri wa kutambulisha wachezaji katika muda rafiki kwa sababu inawathamini mashabiki na wanachama wake.

Simba ilimaliza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/2022 katika nafasi ya pili wakati kwenye mashindano ya Kombe la FA ilitolewa hatua ya nusu fainali kwa kufungwa na watani zao Yanga huku kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika iliishia robo fainali.

# Yanga yaanza hesabu za CAF

## ●●● Bosi atamba hawatarudia makosa ya msimu uliopita huku akisisitiza Mayele hauzwi...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kumaliza msimu wa 2021/2022 kibabe, uongozi wa Yanga umesema mchakato wa uchaguzi unaoendelea ndani ya klabu yao hautaathiri kwa namna yoyote maandalizi ya timu kuelekea katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki.

**Yanga imemaliza msimu kwa kuchukua Ngao ya Jamii, taji la Ligi Kuu ya Tanzania Bara na Kombe la FA, ambayo yote yalikuwa yanashikiliwa na watani zao, Simba.**

Akizungumza jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Senzo Mbatha, alisema licha ya klabu kuwa katika mchakato wa uchaguzi, sekretarieti ya klabu hiyo imejiandaa kukamilisha shughuli mbalimbali za kiutawala ili kutoharibu programu zilizoandaliwa.

Senzo alisema kamwe mchakato huo wa uchaguzi hauna nguvu ya kuathiri mikakati yao kwa sababu wanahitaji kuona Yanga inafanya maandalizi sahihi kwa ajili ya kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika michuano ya kimataifa na ligi watakayoshiriki.

Alisema timu yao inatarajia kwenda Uturuki kwa ajili ya kufanya maandalizi ya msimu ujao na wanaamini kambi hiyo itawaimarisha na kuwajenga nyota wake ili kukabiliana na ushindani watakaokutana nao.

Aliongeza kuhusu usajili tayari Yanga inaelekea kwenye hatua ya mwisho na inawataka wanachama na mashabiki wake kuwa watulivu kwa sababu imezingatia mapendekezo ya benchi la ufundi.

"Suala la usajili halina mashaka kwa sababu tayari tumeshakamilisha kwa asilimia 80, na kazi iliyopo kwetu ni kuangalia ni sehemu gani ambayo timu itaenda kuweka kambi kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kujiandaa na msimu ujao.

"Kila kitu kipo vizuri, kilichobakia ni muda wa kutambulisha wachezaji na kwa asilimia kubwa tumefanya usajili kulingana na mahitaji ya kocha Nabi (Nesredine ), hasa kuangalia zaidi kufanya vizuri zaidi katika michuano ya kimataifa ," alisema Senzo.

Aliongeza kwa sasa wanahitaji kujipanga kuendelea pale walipoishia na ni kupeperusha vizuri bendera ya klabu yao katika Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa.

"Msimu ujao tunahitaji kulinda haya makombe yetu kwa kujipanga vizuri, lakini msimu huu haukuwa mzuri katika michuano ya kimataifa, tumejifunza kitu na tunaenda kufanyia kazi pale tulipokosea na msimu ujao tutafika mbali katika michuano ya Afrika," alisema Senzo.

Ofisa huyo alisema changamoto waliyokuwa nayo msimu uliopita kwa kushindwa kutumia baadhi ya wachezaji wao wa kigeni kwa sababu hati zao za uhamisho za kimataifa (ITC) zilichezewa, kitu hicho hakitajirudia.

Yanga itaanza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika katika hatua za awali huku ikifurahia kupatikana kwa wachezaji wake wa kimataifa ambao ni Yannick Bangala, Fiston Mayele na Khalid Aucho, waliokosekana msimu huu ambao walitolewa mapema.

Mbali na Yanga, timu nyingine kutoka Tanzania Bara zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa ni Simba itakayochuana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Azam FC na Geita Gold FC kutoka mkoani Geita zenyewe zitaenda kuchuana katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Wakati huo huo, mgombea wa nafasi ya urais, Hersi Said amesema mshambuliaji wao, Fiston Mayele hatauzwa na kuwataka mashabiki wa Yanga kutokuwa na hofu.

Hersi alisema pia suala la nidhamu ya wachezaji litaimarishwa na litaendelea kusimamiwa na menejimenti ya klabu na kuahidi mambo mazuri yataendelea kuwamo ndani ya klabu yao katika msimu ujao.

Yanga itafungua msimu mpya kwa kucheza na Simba katika mechi ya kuwania Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 13, mwaka huu wakati Agosti 17, mwaka huu kipenga cha msimu wa 2022/2023 kitaanza rasmi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >